MIAKA 3 YA SAMIA

**The** Royal Tour yapaisha mapato rekodi kihistoria

UKURASA 3



**Timu** uchunguzi yataja ilichobaini madai mfungwa kubaka kijijini

UKURASA 19



**Mfuko** wa SELF wabeba jukumu kukabili kasi ya mikopo umiza

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

Jumanne Machi 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581613

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**GUARDIOLA AELEZA HASIRA YA DE BRUYNE KUTOLEWA**

UKURASA 22

# Ni bajeti ya uchaguzi, viwanja vipya AFCON

• **Yaambatana** na dondoo zenye mapya na ya zamani... *Endelea ukurasa 2*

**Tril. 49.34/-**

**Kiasi ambacho serikali inatarajia kukusanya na kutumia mwaka wa fedha 2024/25**

> **Serikali itaendelea kuhakikisha fedha za mikopo zinaelekezwa kwenye miradi ya kimkakati yenye matokeo ya haraka na manufaa mapana kwa taifa ikiwamo kuongeza fursa za ajira na wigo wa mapato ya serikali...**




## Mgomo endelevu daladala Mwanza, wahamisha ulaji kwa bajaj 9,000

UKURASA 4



## Kasi ya kuvuka gari lingine yaua watu tisa

UKURASA 4

**MICHEZO** KAKOLANYA AIANIKA SIMBA LIGI KUU LEO UK.24 **KATUNI** UK.6

SURA YA 2024/25

# Ni bajeti ya uchaguzi, viwanja vipya AFCON

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



SERIKALI imeweka wazi mfumo na ukomo wa bajeti yake kwa mwaka 2024/25, ikitaja maeneo manane ya kipaumbele ikiwamo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, Uchaguzi Mkuu 2025 na ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, serikali katika mwaka ujao wa fedha inatarajiwa kukusanya na kutumia Sh. trilioni 49.34.

Waziri huyo amebainisha kuwa misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo itapungua kwa asilimia 6.1 kutoka Sh. trilioni 5.4 mwaka 2023/24 hadi Sh. trilioni 5.1.

Akiwasilisha kwenye mkutano wa wabunge jijini hapa jana mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2024/25, Waziri Mwigulu alisema mapendekezo hayo ya bajeti ni sawa na ongezeko la asilimia 11.2 kulinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24 ya Sh. trilioni 44.38.

Alisema makadirio ya mapato kwa mwaka 2024/25 yamezingatia vigezo mbalimbali ikiwamo mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato; mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla; na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya ndani.

Waziri Mwigulu alisema sehemu kubwa ya bajeti (asilimia 70.1) itagharamiwa na mapato ya ndani ambayo yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 10 mwaka 2024/25.

"Serikali itaendelea kuweka msukumo na jitihada za kuimarisha ukusanyaji mapato ya ndani kwa kuwa ndicho chanzo chenye uhakika na kisicho na masharti hasi katika kugharamia bajeti ya serikali," alisema.

Waziri huyo alisema kwa mwaka huo, serikali inakadiria kukopa Sh. trilioni 6. 61 kutoka soko la ndani na Sh. trilioni 2.98 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia utekelezaji miradi ya ujenzi wa miundombinu.

"Serikali itaendelea kuhakikisha fedha za mikopo zinaelekezwa kwenye miradi ya kimkakati yenye matokeo ya haraka na manufaa mapana kwa taifa ikiwamo kuongeza fursa za ajira na wigo wa mapato ya serikali na kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati," alisema.

**MIKOPO YA ELIMU**

Katika mwaka 2024/25, Dk. Mwigulu alisema Sh. trilioni 33.55 zitatumika kwa matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 15.78 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na ongezeko la asilimia 3.8.

Pia alisema fedha za maendeleo zinajumuisha ruzuku ya maendeleo ya Sh. trilioni 1.23 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya kati na ya juu pamoja na programu ya elimumsingi na sekondari bila ada, maarufu elimu bure.

Alifafanua kuwa sehemu kubwa ya matumizi itaelekezwa katika kugharamia Deni la Serikali, mishahara ya watumishi wa umma, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 2025, ulipaji hati za madai na ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya AFCON 2027, huduma za jamii na sekta za uzalishaji.

Waziri huyo alisema utengaji fedha za maendeleo umezingatia miradi inayoendelea ikiwamo miradi ya kimkakati na ya kielelezo pamoja na utekelezaji miradi kupitia utaratibu wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi (PPP) ili kuipunguzia serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka.

Ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji bajeti ya 2024/25, Dk. Mwigulu alisema sera za mapato na hatua za kiutawala kwa mwaka 2024/25 zitalenga kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero.

Alisema wataboresha pia mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari, kuongeza wigo wa kodi, kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji mapato, hususan kodi ya ardhi na pango.

Katika mwaka 2024/25, Dk. Mwigulu alisema serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikijumuisha mishahara na Deni la Serikali.

Pia alisema serikali itaendelea kugharamia matumizi ya maendeleo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji na Wakala wa Maji Vijijini.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai pamoja na kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na kuendana na thamani ya fedha.

# Programu 162 zaja kukuza uchumi na kuzalisha ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja sekta zinazokua kwa kasi kubwa na shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa mwaka 2023 huku ikitoa uelekeo wa miradi na programu 162 zitakazotekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25.

Lengo la mpango huo ni kuchochea kasi ya ukuaji uchumi ambao ni jumuishi, unaopunguza umaskini na kuleta ustawi kwa wote, unaozalisha ajira kwa wingi na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

Akiwasilisha kwenye mkutano wa wabunge jana mapendekezo ya serikali ya mpango huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema katika tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi, inaonesha Pato la Taifa liliongezeka kutoka Sh. trilioni 124.2 katika kipindi cha Januari – Septemba 2022 hadi kufikia Sh. trilioni 140.0 katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2023.

Alisema uchumi wa taifa ulikua kwa asilimia 5.3 katika kipindi cha Januari – Septemba 2023 kulinganisha na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

"Sekta zilizokua kwa kasi kubwa katika kipindi cha marejeo ni pamoja na: Fedha na bima (asilimia 16.0); uchimbaji madini na mawe (asilimia 10.2); umeme (asilimia 10); huduma nyingine ikijumuisha sanaa na burudani (asilimia 10); malazi na chakula (asilimia 8.9); na habari na mawasiliano (asilimia 7.9)," alisema.

Waziri huyo alisema katika kipindi hicho shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ni pamoja na kilimo (asilimia 24.8), ujenzi (asilimia 13.6), uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.7), biashara na matengenezo (8.4), uchukuzi na uhifadhi wa mizigo (asilimia 7.2) na viwanda (asilimia 6.9).

Kuhusu miradi na programu katika mpango wa maendeleo kwa mwaka ujao, Prof. Kitila alisema katika kuchochea ushindani wa kiuchumi na ukuaji wa uchumi jumuishi, programu na miradi 100 itatekelezwa ambayo ni miradi ya kielelezo, ikiwamo mradi wa reli ya kisasa (SGR) na miradi ya kufua nishati ya umeme kama vile Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Rufiji, Rusumo, Rumakali, Kinyerezi na miradi ya umeme wa jua na upepo.

Pia alisema wataendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga na majini, utunzaji endelevu wa mazingira na nchi inaimarisha matumizi ya gesi (CNG) katika uendeshaji magari ili kuanza kupunguza utegemezi wa mafuta ya kuagiza nje ya nchi.

"Tutaendelea pia kuongeza tija katika uzalishaji mazao ya kilimo, kuongeza thamani mazao, kukuza na kuimarisha uwezo wa kutunza mazao katika kuimarisha usalama wa chakula na kukuza masoko ya mazao ya wakulima.

"Serikali itachukua za kuendelea kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora hususani kwa mazao ya kimkakati," alisema.

Waziri huyo alitaja miradi mingine ni kuimarisha huduma za ugani, kupanua kilimo cha umwagiliaji, ikiwamo kukamilisha skimu 25, kukarabati skimu 30 na kukamilisha ujenzi wa mabwawa 14 ya kuvuna maji ya mvua, kuimarisha upatikanaji pembejeo kwa wakulima, ikiwamo kununua magari matano yenye uwezo wa kubeba tani 30 za mbegu, kujenga maabara mbili za mbegu, kununua vifaa vya utafiti na kujenga maghala matatu ya kuhifadhi mbegu.

"Pia kuendelea kutekeleza programu ya BBT kwa kutambua na kuainisha mashamba mapya 30 katika mikoa mitano, kupima ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji katika mikoa 10, kutoa mafunzo kwa walengwa 1,000, kutoa mikopo ya riba nafuu kwa vijana na wanawake na kuhamasisha uanzishwaji kampuni za ugani kwa kushirikisha vijana wanaohitimu mafunzo ya kilimo," alisema.

Pia alisema wataweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani (primary processing) katika sekta za kimkakati, zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi na misitu.

"Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali (semi-processed).

"Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Kuendelea kuhamasisha, kutangaza na kuwezesha uwekezaji, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi," alisema.

Pamoja na hayo, waziri huyo alisema watapitia upya mfumo wa kodi ili kuweka mazingira ya kukua kwa wigo wa walipakodi sambamba na ukuaji wa Pato la Taifa, kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu, kuzingatia umuhimu wa dijitali katika kuleta mapinduzi ya uchumi vijijini.

"Serikali itaanzisha mradi wa kujenga mfumo wa dijitali vijijini ili kuunganisha wananchi vijijini katika uchumi wa taifa na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kiuchumi na kijamii," alisema.

Waziri Mkumbo alisema kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya nje, serikali itaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini, hususani katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo.

Prof. Mkumbo alisema katika kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii, programu na miradi 62 itatekelezwa ikiwamo kuendelea na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya pamoja na upatikanaji wa vifaa tiba.

Alisema pamoja na hatua kubwa serikali iliyopiga katika kutokomeza ugonjwa wa malaria, ugonjwa huo unaendelea kuwa tishio kwa afya za wananchi, hivyo serikali itaelekeza nguvu katika programu za kuangamiza mazalia ya mbu.

Alisema wataendelea kutekeleza miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira, ikiwamo kuendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa kusafirisha maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Singida na Dodoma kwa ajili ya maji safi ya kunywa na umwagiliaji.

Alisema wataendelea na upanuzi na uboreshaji miundombinu ya kujifunza na kujifunzia, pamoja na upatikanaji vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu.

"Serikali itaendelea na utekelezaji programu ya kutoa elimu ya msingi na sekondari bila ada, kutoa mikopo kwa wanafunzi 93,500 wa elimu ya juu na elimu ya kati, wakiwamo wanafunzi 10,000 wa mafunzo ya stashahada, kutekeleza sera na mitaala mipya ya elimu, ikiwamo mafunzo kwa walimu," alisema.

# Utalii na siri ya kuongezeka nchini

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

ALIANZA kwa kuigiza filamu ya 'The Royal Tour', akijua mapema matokeo ya uhusika wake katika filamu hiyo itakavyochochea ukuaji wa sekta ya utalii nchini.

Ndivyo inavyoweza kuelezwa, baada ya miaka mitatu madarakani ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuufanya utalii wa Tanzania kupaa maradufu.

Taarifa za hali ya uchumi za robo ya mwisho ya mwaka 2023 (Quarterly Economic Review) ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaonesha namna watalii walivyomiminika chini.

Katika kipindi chake cha uongozi, hadi kufikia mwishoni mwa waka jana, watalii walioingia nchini walikuwa 1,790,301.

Kiwango hicho, ni cha juu zaidi kuwahi kufikiwa katika sekta hiyo tangu uhuru.

Kupitia taarifa za hali ya uchumi za sekta ya utalii, na za Bunge, sekta ya utalii imeliingizia taifa fedha za kigeni, zaidi ya Dola za Marekeni bilioni 3.3, sawa na zaidi ya asilimia 25 ya mauzo yote ya nje nchini hadi kufikia Desemba 31, 2023.

Sekta ya utalii ndiyo iliyoongoza Tanzania katika kuingiza fedha za kigeni, huku ikiwa imechangia zaidi ya asilimia 20 ya Pato Ghafi la Taifa (GDP).

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya Mwaka 2023, kwa upande wa ajira, sekta ya utalii imeongeza ajira za moja kwa moja kufikia hadi ajira milioni 1.6, sawa na asilimia 11 ya ajira nchini.

Taarifa za kamati hiyo ya Bunge zinaonesha umahiri wa Rais Samia alivyofanikiwa kuutangaza utalii wa Tanzania nje ya mipaka yake.

Katika ripoti hiyo, miongoni mwa wageni waliotembelea Tanzania kwa lengo la kutalii, asilimia 58 huvifikia vivutio vya Hifadhi za Taifa na asilimia 42 hutembelea maeneo mengine ya utalii, ikiwamo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na fukwe za Zanzibar.

Mathalani, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), imeweka wazi kuwa Rais Samia katika miaka yake mitatu madarakani, amefanya mengi ya kuacha alama katika kuhakikisha taifa linafikia lengo la watalii milioni tano kwa mwaka 2025 na fedha za kigeni zaidi ya Dola za Marekeni bilioni sita.

Katika eneo hilo la kutangaza utalii na vivutio vyake, Rais Samia amepiga hatua moja mbele kwenye mikakati mahsusi ya kupanua wigo wa masoko ya utalii ya kimkakati, ikiwamo nchi za Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (BRICS).

Mkakati huo umelipa taifa picha halisi ya anachokifanya Rais Samia, kitakavyokuwa na matokeo chanya, hasa katika mazao mbadala ya utalii, ambayo ni pamoja na utalii wa kihistoria, utamaduni na utalii wa fukwe, ambao nchi imebarikiwa kuwa na rasilimali hizo.

Mikakati mingine aliyofanikiwa Rais Samia, ni kutangaza utalii kupitia watu mashuhuri kutoka kwenye masoko ya nchini.

Mfano China, Rais Samia na serikali yake, imefanikiwa kuja na mpango wa kuwatumia Lu Han anayefuatiliwa katika mtandao wa kijamii wa Instagram na watu milioni 10.9 na Jing Dong (15k Instagram followers) na Priyanka Chopra (89.9m Instagram followers).

Kwa mujibu wa TTB, Rais Samia aliagiza kazi hiyo ipewe msukumo zaidi katika mwaka wa fedha 2024/25 - 2025/2026, ili kuongeza idadi ya watalii wa nje wanaofuatilia vivutio vya Tanzania.

Kutokana na matokeo mazuri ya kushangaza ya Filamu ya The Royal Tour, iliyofanywa na Rais Samia, sasa Bodi ya Utalii Tanzania, inapanga kuratibu uzalishaji wa filamu nne za kimataifa.

Katika kipindi chake cha uongozi, serikali inapanga tena kurekodi filamu mbili za mwendelezo wa 'The Royal Tour' na makala mbili za video za kimataifa kutoka kwa wazalishaji wa viwango vya Hollywood.

Filamu hizo, moja itaitwa Kijiji cha Milele au Presidential Tour iliyomshirikisha Rais Samia, na mwigizaji maarufu wa filamu, Jing Dong kutoka nchini China.

Na nyingine ni maandalizi ya documentary (makala maalum) inayohusu mchango wa Mwalimu Julius Nyerere katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Mbali na kuchochea ukuaji wa sekta hiyo, pia Rais Samia, amejipambanua kwa kutekeleza miradi ya maendeleo sita iliyopo katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kushuka ndani ya Kreta (Seneto Descend Road) katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Pia, ameanzisha Mradi wa Uwanja wa Ndege na jengo la kupokea wageni katika Hifadhi ya Taifa Tarangire na Mradi wa Ukarabati wa Maonyesho na Maktaba katika eneo la Azimio la Arusha na Elimu Viumbe.

Kwa dhamira yake, sekta ya utalii sasa ina mchango mkubwa katika ustawi wa wananchi, ukuaji wa uchumi na kuwa sekta inayohakikisha uchumi wa nchi unakuwa stahimilivu kwa wakati wote kwa kuchangia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni, kuliko sekta zote za uchumi nchini.

Jambo la kupigiwa mfano, ni dhamira yake njema ya kuinusuru Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), kupoteza uhalisia wake katika kuvutia utalii nchini.

Licha ya sheria iliyounda Ngorongoro, Rais Samia anapambania kuweka msingi wa shughuli zinazozingatia uhifadhi, ili kulinda ikolojia ya eneo la Ngorongoro, ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama na vyanzo vya maji katika eneo la hifadhi.

Kutokana na ongezeko la watu na shughuli za binadamu, ikiwamo ufugaji na kilimo, Rais Samia aliamua kuwashawishi wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro na Sale walioko ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kuanza kuhama kwa hiari ili kupisha shughuli za uhifadhi.

Rais Samia alimua kuchukua hatua hiyo ili kukuza sekta ya utalii nchini, na kuepusha ushindani wa rasilimali, kati ya wakazi wa eneo la hifadhi na viumbe hai wengine kwenye hifadhi.

Eneo hilo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ni moja ya eneo la urithi wa dunia, lipo hatarini kupoteza ikolojia yake.

Kazi ya kuwahamisha wakazi wa Ngorongoro kwa hiari, ilianza Februari, 2022 ikiwa ni awamu ya kwanza iliyokamilika mwezi Julai, 2023.

Utekelezaji wa mradi wa kuhamisha wananchi waishio eneo la Hifadhi ya Ngorongoro awamu ya pili, ulianza Julai, 2023.

Vipengele vya mradi katika awamu hii vinahusisha; ujenzi wa nyumba 5,000, ujenzi wa miundombinu ya huduma za kijamii, kutoa elimu na uhamasishaji.

Mambo mengine aliyoyafanya Rais Samia na serikali yake, ni kuwezesha uthamini wa mali na kuhamisha kaya zilizojiandikisha kuhama kwa hiari kwenda vijiji vya Msomera (Handeni), Kitwai (Simanjiro) na Saunyi (Kilindi) na maeneo mengine wanayochagua wananchi wenyewe.

Awamu ya kwanza serikali ya Rais Samia, ilijenga nyumba 503 katika Kijiji cha Msomera na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na jumla ya watu 3,010 na mifugo 15,521.

Kadhalika, Rais Samia ameiinua Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Nchini (TAWA), baada ya kuwekeza zaidi utaalamu na vifaa katika tasnia ya uwindaji wa kitalii, kufanyika kwa madhumuni ya kupata burudani na kupata nyara.

Hapa nchini, uwindaji huu wa kitalii huchangia fedha za kigeni, ambapo serikali hukusanya takribani Dola za Marekani milioni 12.8 kwa mwaka kutokana na uwindaji wa kitalii.

Vilevile, huchangia zaidi ya asilimia 60 ya mapato ya TAWA. Wakati, Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), Rais Samia ameibeba ajenda ya utalii kwa kuhakikisha bajeti yake haitetereki.

Hadi sasa TANAPA inasimamia Hifadhi za Taifa 21, zikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 96,908.88 sawa na takribani asilimia 10.2.

Kwa msingi huo, ameendelea kuipa sapoti kubwa TANAPA kuzilea pamoja Hifadhi za Taifa 16 zilizokuwapo awali, kuendelea kusimamia maeneo ya hifadhi mpya za taifa tano zilizoongezeka.

Hifadhi mpya zilizoongezeka na ambazo Rais Samia ameziwekea msukumo mkubwa wa kuzitangaza ili zijulikane kimataifa ni Burigi/Chato, Ibanda/Kyerwa, Rumanyika/Karagwe, Mto Ugalla na Nyerere.

Kuhusu usimamizi wa Maliasili Endelevu na Ukuaji wa Utalii Kanda ya Kusini (REGROW), Rais Samia, amefanikiwa kuusimamia vizuri mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 150, sawa Sh. bilioni 345 kutoka Benki ya Dunia (WB).

Mradi huo uliopangwa kukamilika Septemba 2023, uliongezewa muda wa miezi 17, na sasa utakamilika Februari 28, 2025.

Amefanikiwa zaidi kusimamia mradi kutekelezwa kwenye maeneo ya kipaumbele yaliyohifadhiwa kusini mwa Tanzania, ambayo ni Hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na Nyerere, na Hifadhi ya Msitu Asili wa Kilombero.



**Katika eneo hilo la kutangaza utalii na vivutio vyake, Rais Samia amepiga hatua moja mbele kwenye mikakati mahsusi ya kupanua wigo wa masoko ya utalii ya kimkakati, ikiwamo nchi za Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (BRICS).**



Watumishi wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini wakiweka tuta katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam juzi ili kuzidhibiti gari zinazokwenda kasi kwenye maeneo ya wakazi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasi ya kuvuka magari mengine yaua watu tisa

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WATU tisa wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa katika ajali iliyotokea Machi 10, mwaka huu katika eneo la Kiromo, Bagamoyo mkoani Pwani umbali wa kilomita 60 kwenda Dar es Salaam ikihusisha magari mawili kugongana uso kwa uso.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Pius Lutumo, alisema ajali hiyo ilitokea majira ya saa 11:15 jioni.

Kamanda Lutumo alisema gari aina ya Toyota Costa yenye namba za usajili T676 DSM likiendeshwa na Juma Mackey ikitokea jijini Dar es Salaam kuelekea Bagamoyo, iligongana uso kwa uso na lori aina ya HOWO CABEN lenye namba za usajili T 503 DRP na Trela T 733 DUQ lililokuwa likiendeshwa na Apolo Mgomela.

Alisema ajali hiyo imetokea baada ya lori hilo lililokuwa limebeba mawe kutaka kuyapita magari mengine, bila kuchukua tahadhari na kwenda kukutana uso kwa uso na Costa.

Alisema waliokufa katika ajali hiyo ni wanaume saba na wanawake wawili, huku majeruhi wakiwa ni wanaume wawili na mwanamke mmoja akiendelea na matibabu Hospitali ya Wilaya Bagamoyo na miili ya marehemu imehifadhiwa katika hospitali hiyo.

Lutumo alisisitiza madereva na watumiaji wa barabara kuwa makini kwa kuzingatia sheria za barabarani.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alifika kwenye eneo la tukio na kutoa pole kwa majeruhi pamoja na waliopoteza ndugu zao kwenye ajali hiyo.

Desemba mwaka jana, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilitoa taarifa ya ajali nchini na kuonesha kuwa kati ya ajali 1,641 zilizotokea barabarani, kwa kipindi cha Januari Mosi hadi jana (Desemba 12) na kusababisha vifo vya watu 1,550 miongoni mwao wanaume waliofariki dunia walikuwa ni 1,189 huku wanawake wakifariki 361.

Aidha, majeruhi 2,562 wa ajali kwa kipindi hicho, wanaume ni 1,721 huku wanawake wakiwa 841 na madereva 1,226 wakifikishwa mahakamani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo mwaka jana, mkoani Dar es Salaam, mbele ya waandishi wa habari, baada ya kuhitimisha kikao na wadau wa usalama barabarani.

Kikao hicho kililikutanisha Baraza la Usalama Barabarani na kuhudhuriwa wadau mbalimbali, wakiwamo maofisa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.

Alifafanua takwimu za ajali kwa kipindi cha miezi 12, mwaka huu, akisema mbali na vifo kwa kipindi hicho, ajali 1,641 kati yake, zilisababisha uharibifu wa vyombo vya moto 135.

“Madereva waliofungiwa leseni kwa kipindi hicho ni 2,596 kutokana na makosa mbalimbali,” alisema Masauni.

# Mgomo endelevu daladala Mwanza, wahamisha ulaji kwa bajaji 9,000

**Na Waandishi Wetu**

WAMILIKI wa vyombo vya usafiri wa umma mjini maarufu ‘daladala’ pamoja na madereva mkoani Mwanza wamegoma kufanya shughuli za usafirishaji jana wakishinikiza serikali kuondoa pikipiki za magurudumu matatu maarufu ‘bajaji’ maeneo ya mjini.

Mgomo huo ulioanza jana ulisababisha adha ya usafiri kwa abiria hususani wanafunzi wanaotegemea huduma hiyo majira ya alfajiri kutoka maeneo mbalimbali walishindwa kwenda shuleni kutokana na gharama za bajaji na pikipiki za mizigo zilizokuwa zikitoa huduma hiyo huku wengine wakichelewa.

Mgomo huo ulisababisha kupanda kwa nauli ya pikipiki ‘bodaboda’ kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 2,000 na kwa usafiri wa bajaji kutoka Sh. 500 hadi Sh. 1,000 hali iliyosababisha wanafunzi na raia wengine kupanda usafiri unaotumika kubeba mizigo na wengine kutembea kutoka sehemu wanazoishi hadi maeneo ya kazi.

Mwanafunzi Monira Hashimu, aliiambia Nipashe kuwa alishindwa kuendelea na safari ya kuelekea shuleni baada ya kukosa usafiri huku akishindwa kwenda na usafiri mbadala kutokana na bajeti aliyotoka nayo nyumbani na kulazimika kurudi ili kuandaa utaratibu mwingine.

Baadhi ya wachuuzi wa dagaa katika mwalo wa Mswahili jijini hapa akiwamo Mariam Hamis, alisema walilazimika kutembea kufuata mzigo mwaloni kisha kurejea katika shughuli zao kutokana na kushindwa kumudu gharama za bajaji ambazo walizitaja kuwa kubwa zaidi ya faida ya biashara zao.

Neema Omary msaidizi wa kazi za ndani ambaye anajukumu la kumpeleka mwanafunzi shuleni kila asubuhi, alisema eneo la kusafiri kwa Sh.600 alitumia Sh. 1,500, hata hivyo, alimfikisha mwanafunzi huyo kwa kuchelewa.

Akizungumza na Nipashe, dereva wa daladala, David Ishengoma, alitaja sababu ya mgomo huo kuwa ni ongezeko la bajaji maeneo ya mjini zinazofanya kazi ya kupakia na kushusha abiria bila mpangilio wakiitaka serikali kuingilia kati tatizo hilo.

“Tumechoshwa na hii hali ya kuingiliwa katika kazi zetu na serikali haichukui hatua yoyote kwani watu hao (bajaji) wana leseni za kukodishwa na siyo kama wanavyofanya kwa sasa tuliwahi kupeleka maombi kwenye mamlaka husika ya hizi bajaji kuwekewa utaratibu mzuri wa njia zao.”

“Pia ijulikane zinaanzia wapi na kuishia wapi, lakini hayakufanyiwa kazi mpaka hali inafikia tunakosa abiria wa kupakia, abiria wote wanaenda kupanda bajaji na unakuta unapaki gari hata dakika 15 hadi abiria walioko kwenye gari wanaanza kulalamika kuwa tunawachelewesha wanakokwenda,” alisema David.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Daladala Mkoa wa Mwanza, Mjarifu Manyasi, alisema ni mgomo huo ni endelevu mpaka tatizo hilo lipatiwe ufumbuzi.

“Madereva wanashindwa kukamilisha hesabu za bosi na kusabisha mizozo kutokana na wingi wa bajaji mjini na pembezoni ambao wanapakia abiria hadi kwenye vituo vya daladala huku mamlaka husika zikiendelea kukaa kimya,” alisema Mjarifu.

Alisema wameshaunda kamati ya kufuatilia tatizo hilo na mamlaka zimekuwa zikiwasihi waendelee kutoa huduma lakini wameshindwa kuvumilia wakidai mgomo huo utaendelea mpaka watakapo pata mwafaka kutoka kwa viongozi wanaohusika na masuala ya usafirishaji ikiwamo Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana na Ilemela.

Meneja Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Mwanza, Halima Lutavi alipotafutwa kwa njia ya simu,

ilipokewa na msaidizi wake aliyejitambulisha kwa jina moja la Hafidhi na kueleza kuwa jambo hilo linafanyiwa kazi.

Alisema ufumbuzi wake unaendelea kufanywa na mamlaka hizo kwa kushirikiana na mamlaka zingine, wamiliki wa daladala wanatambua mchakato unavyoendelea mpaka sasa.

Vilevile, alisema Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wote wana taarifa na wanajua kinachoendelea na wanalifanyia kazi suala hilo na muda si mrefu kila kitu kitakuwa sawa.

Kutokana na mgomo huo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alitoa saa mbili daladala hizo kurudi barabarani na kwamba ufumbuzi wa tatizo hilo unaendelea. Licha ya agizo hilo mgomo uliendelea, madereva hao wakidai kuchoshwa na maelekezo ya mara kwa mara.

Kutokana na kuendelea kwa huo uliowakusanya madereva hao pamoja katika viwanja vya Furahisha wakiendelea kushinikiza serikali kuchukua hatua za haraka kutatua tatizo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, alifika viwanjani hapo kuwasikiliza madereva hao na kuwasihi kuendelea kutoa huduma na kuwaomba kuwavumilia kwa kipindi cha mwezi mmoja na nusu watakuwa tayari wameziondoa daladala mjini.

Alisema kwa Mkoa wa Mwanza zipo bajaji zilizosajiliwa zaidi ya 9,000 huku vituo vilivyotengwa kwa ajili ya watoa huduma hao vikiwa ni 16 pekee ambavyo havikidhi uhitaji wao.

Aidha, baadhi ya waendesha bajaji mkoani hapa akiwamo Samson Mussa, alisema hawachangamani na daladala kwa kuwa wanabeba abiria wengi wakati bajaji zinabeba abiria watatu kwa gharama tofauti na daladala.

“Wao wakiamua kuendelea na mgomo waendelee sisi kwetu ni faida washinikize serikali labda itawasikiliza, lakini sisi hatuna tatizo lolote na wao,” alisema Mussa.

***Imeandaliwa na Neema Emmanuel, Rose Jacob, Zatifa Ramadhan na Vitus Audax (MWANZA)**

# SELF yaandaa mwarobaini wa mikopo umiza kwa wananchi

Na Jenifer Gilla

MFUKO wa Fedha wa SELF umesema unaendelea kutanua wigo wa utoaji mikopo nchini ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi, kwa ajili ya kuwaepusha na wakopeshaji binafsi wanaowakopesha kwa masharti magumu maarufu kama kaushadamu au mikopo umiza.

Mfuko huo unaomilikiwa na serikali unajihusisha na utoaji mikopo kwa wafanyabiashara wa chini na kati, unajivunia kuwafikia zaidi ya wakopaji 300,000 katika matawi 12 nchini.

Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo ya kiserikali, Mudith Cheyo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuhusu utekelezaji wa shughuli zao kwa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kwa sasa wananchi wengi wanakwenda kwenye mikopo binafsi yenye majina mengi (mikopo umuza, kausha damu) ambayo ina masharti magumu, na kwamba wamejipanga vyema kuhakikisha wanakuwa kimbilio kwa wahitaji.

Cheyo alisema taasisi hizo zimekuwa zikitoa mikopo kwa wafanyabiashara kwa masharti magumu bila ya kuwachunguza uwezo wao na kuwapa elimu ya ujasiriamali, hali inayowapelekea kushindwa kulipa deni kwa wakati na kuwafilisi.

Alisema mfuko huo kabla ya kumpa mteja mkopo wanatumia muda kumchunguza na kumjua zaidi kwa kuangalia mambo mbalimbali ikiwamo nia yake ya kutaka mkopo, uwezo wa kuendesha biashara anayoichukulia mkopo, wanahitaji kujengewa uwezo gani ili afikie malengo yake na alipe rejesho kwa wakati.

Alisema kwa takribani nane waliotoa huduma hiyo, wamegundua kuwa baadhi ya wanakwenda kukopa hawana elimu ya fedha, wanaendesha biashara zisizo rasmi na wengine hawana utamaduni wa kukopa hali inayopelekea kuchukua pesa na kufanyia mambo yao binafsi badala ya lengo kusudiwa.

Kwa mujibu wa Cheyo, wanakabiliana na hali hiyo kwa kuwapa elimu ya fedha ya na kumwongoza katika biashara yake ili kuhakikisha fedha alizochukua wapeleke kwenye malengo kusudiwa.

"Wakati mwingine tunagundua kuwa mteja wala haitaji mkopo bali anahitaji msaada na usimamizi wa kuendesha biashara aliyonayo kwa mtaji alionao, kwa hiyo tunampatia anachohitaji," alisema.

Mkurugenzi wa Biashara, Petro Mataba alisema mfuko huo ulianzishwa mwaka 2015 na kupewa ruzuku na Sh.bilioni 56 na serikali na sasa wamefikisha Sh. bilioni 62 na sasa wanalipa gawio la zaidi ya Sh. milioni 200 kwa serikali, mwaka ulioisha 2023 walipata faida ya Sh. bilioni 2.

Alisema hadi kufikia Decemba, 2023 mfuko ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya Sh. 324,506,402,014, ikiwa na kiwango cha mikopo chechefu chini ya 10% na kuzifia taasisi binafsi 314,055 kati ya milioni 4 zinazohitaji kupata huduma hizo.

"Kati yao wanawake 166,449 sawa na asilimia 53 na wanaume 147,606 sawa na asimia 47. Wanufaika hao wanatoka katika mikoa 30 ya Tanzania Bara na Visiwani."

Mkurugenzi wa Masoko, Santiel Yona, alisema, ndoto ya mfuko huo ni kwa miaka 25 ijayo kuwa na matawi katika mikoa yote nchini Tanzania, ili kuwafikia wafanyabiashara wengi hasa wadogo ambao huishia kufilisiwa kwa kukopa sehemu zisizoendana na uwezo wao.

Aliitaja maeneo ambayo wameifikia mpaka sasa kuwa ni Dar es Salaam, Zanzibar, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Katavi, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Geita, Kagera, Kigoma, Mtwara, Lindi, Tanga, Mwanza,Simiyu, Mara, Iringa, Njombe, Ruvuma, Dodoma , Singida, Mbeya, Songwe na Rukwa.

## ...FCC yaonya wananchi wanaokopa kausha damu

Na Faustine Feliciane

WAKATI wakijiandaa kufanya maadhimisho ya Siku ya Haki kwa Mlaji Duniani, Tume ya Ushindani (FCC), imewaonya wananchi kuacha kuchukua mikopo kwa taasisi au watu binafsi bila kujua masharti ya mkataba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa maadhimisho hayo ambayo kilele chake ni Machi 15, Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Erio, alisema mikataba yote ya mikopo lazima iandikwe kwa lugha inayoeleweka kwa mkopaji, lakini mhusika anapaswa kuelewa na kukubali vipengele vya mikataba hiyo.

Alisema FCC inawashauri wananchi kuchukua mikopo kwenye taasisi zinazotambulika ili kuepuka kutepeliwa na kuingia makubaliano ya mikopo yenye kuwakandamiza.

"Katika maadhimisho ya siku ya haki ya mlaji duniani, FCC tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujua haki zao, lakini pia suala la mikopo ya kausha damu tunawashauri wananchi kujua haki zao, suala la mikopo na maamuzi ya mtu mwenyewe hivyo lazima waangalie na kuulewa mkataba wa kukopeshana," alisema Erio.

Alisema katika maadhimisho ya mwaka huu ya siku ya haki ya mlaji, kaulimbiu ni 'matumizi akili mnemba yanayozingatia haki ya mlaji.'

Aidha, alisema kuelekea kwenye maadhimisho hayo, FCC wameandaa kliniki kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi Machi 13, mwaka huu, pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto katika ofisi za mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza.


**TANDAHIMBA COOPERATIVE BANK LIMITED**

*Wanachama,*

**YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KWANZA WA WANACHAMA**

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wanachama wa Chama cha Tandahimba Coopeartive Bank Limited** utafanyika siku ya Jumanne tarehe **19 Machi, 2024,** katika **Maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika TANECU, Tandahimba** kuanzia saa saba kamili (Saa 7:00) mchana kujadili agenda zifuatazo:

1. **Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mkutano**
2. **Kufungua Mkutano.**
3. **Kuridhia Dondoo za Mkutano.**
4. **Kuwasilisha Cheti cha Usajili wa Chama cha Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
5. **Kupitisha Bajeti anzia ya Chama kwa mwaka 2024.**
6. **Uchaguzi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi wa Chama Cha Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
7. **Azimio Maalum la kupokea Mali na Madeni kutoka Tandahimba Community Bank Plc.**
8. **Azimio Maalum la kuidhinisha kuunganisha Chama cha Tandahimba Cooperative Bank Limited na Kilimanjaro Cooperative Bank Limited.**
9. **Azimio Maalum la kukasimisha mamlaka ya mkutano mkuu kwa Bodi ya Tandahimba Cooperative Bank Limited kukamilisha zoezi la uanzishwaji wa Benki ya Ushirika Tanzania.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kufunga Mkutano.**

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**

**Meneja Mkuu,**
**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC,**
**Kiwanja Na. 49- Kitalu 'C', Barabara ya Namikupa,**
**S. L. P. 06, Tandahimba**
**Mtwara.**
**Namba ya Simu: +255 23 241 0093**
**Barua pepe: info@tacobabank.co.tz**

**KWA IDHINI YA KAMATI**

Yahya Jumanne Kiyabo
**MENEJA MKUU**

**12 Machi, 2024**



TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC TACOBA
"Our Bank for Our Development"

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

**IMERUDIWA**
**YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Kumi wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank Plc** utafanyika siku ya Jumanne tarehe **19 Machi, 2024,** katika **Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU, Tandahimba** kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00) asubuhi** kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita.**
   Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 24/06/2023
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.**
   Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 24/06/2023
5. **Kujadili na kupokea Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2023.**
   **5.1** Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi.
   **5.2** Taarifa ya Meneja Mkuu.
   **5.3** Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Disemba 2023.
6. **Azimio Maalum la kuhamisha Mali na Madeni ya Tandahimba Community Bank Plc Kwenda Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
7. **Azimio Maalum la kuidhinisha kubadili jina la Tandahimba Community Bank Plc kuwa Tandahimba Community Plc.**
8. **Azimio Maalum la kuidhinisha kufungwa kwa kampuni ya Tandahimba Community Plc baada ya kuhamisha mali na madeni kwenda Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
9. **Azimio Maalum la kukasimisha mamlaka ya kusimamia na kutekeleza mchakato wa ufungwaji wa kampuni ya Tandahimba Community Plc kwa Bodi ya Wakurugenzi.**
10. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
11. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
12. **Kufunga Mkutano.**

**MAELEZO**
1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 18/03/2024.*
2. *Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki ya Wananchi Tandahimba tarehe 15/03/2024 na kwenye Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU tarehe 19/03/2024.*
3. *Wanahisa watakaoshindwa kuhudhuria wana haki ya kujaza fomu ya uwakilishi iliyoambatanishwa.*
4. *Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.*

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**

**Katibu**
**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC,**
**Kiwanja Na. 49- Kitalu 'C', Barabara ya Namikupa,**
**S. L. P. 06, Tandahimba**
**Mtwara.**
**Namba ya Simu: +255 23 241 0093**
**Barua pepe: info@tacobabank.co.tz**

**KWA IDHINI YA BODI**

J. B. Rugambo
**KATIBU**

23 Februari, 2024

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kliniki za ardhi zinasaidia kupunguza milolongo kupata hati

**WANANCHI** wana kero nyingi zinazowakabili, lakini wengi wao hawana mwongozo mzuri wa wapi pa kuziwasilisha na kuishia kudhulumiwa na kunung'unika bila tatizo lao kutatuliwa.

Kuna wengi wamepoteza mali zao na vitu vyao vya thamani kwasababu ya kudhulumiwa kwa kuwa waathirika wa mikasa hiyo huishia kuzungushwa bila kupata mwafaka.

Kuna utaratibu ulioanzishwa na Waziri wa Ardhi wa kuweka kliniki za ardhi, ambao umesaidia wananchi wengi waliokuwa na changamoto na migogoro ya viwanja kupata mwongozo wa kutatua tatizo lao.

Kupitia utaratibu huo, Waziri mwenyewe hushiriki kwenye kliniki hizo na kusikiliza kero za wananchi na hatimaye kutoa suluhisho.

Utaratibu huu umewakomboa wananchi wengi na kupata haki zao za kumiliki ardhi na kupata hati za viwanja.

Wizara ya Ardhi imeweka utaratibu huo kila wilaya kwa kutenga maeneo maalumu ya kliniki hizo kila wiki ambazo hujumuisha wafanyakazi wa vitengo vyote vya ardhi wakiwamo wanasheria wa kusaidia msaada wa kisheria.

Kitu kizuri kinachofanyika kwenye kliniki hizo ni kwamba huduma zote zinapatikana sehemu moja badala ya kuhangaika kwenda maeneo mbalimbali.

Kama wizara zote zinazotoa huduma muhimu za kijamii kama ilivyokuwa Wizara ya Ardhi, Tanzania bila migogoro ya ardhi ingewezekana.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, ametangaza kuanzisha utaratibu wa kutenga siku moja kila mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi mmoja mmoja kwa kukutana nao katika ofisi za Chama Cha Mapinduzi zilizopo Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Lengo la Rais Samia, ambaye katika kusikiliza kero atavaa kofia ya Mwenyekiti wa CCM ni kuwaonyesha viongozi wanavyopaswa kuwajibika katika nafasi zao kutatua kero za wananchi.

Rais Samia ameamua kufanya hayo akiwa na maana kubwa ikiwamo kudumisha na kuidhinisha kwa vitendo kwa kuwataka viongozi aliowateua kuwasikiliza na kutatua kero za wananchi.

Kwa hatua hii aliyoichukua Rais Samia, viongozi aliowateua wana la kujifunza na wanapaswa kujiuliza mpaka kiongozi aliyewateua anaamua mwenyewe kutatua kero ambazo zingefanywa na wateule wake, kuna tatizo.

Mara kwa mara viongozi wakuu wanapokuwa kwenye ziara zao na kutoa nafasi kwa wananchi kutoa kero zao, ndipo huibuka malalamiko ambayo yangeweza kushughulikiwa na walioteuliwa kufanya kazi hiyo.

Tumeshuhudia Waziri Mkuu akiibua madudu yanayofanywa kwenye miradi mikubwa inayopaswa kuhudumia wananchi, ambayo inakosa usimamizi wa kutosha na badala yake pesa nyingi kutumika tofauti na mradi wenyewe.


Jambo kubwa la kujiuliza ni vipi viongozi walioteuliwa kushika nyadhifa wanashindwa kusimamia kazi zao mpaka mkuu wa nchi mwenyewe anaamua kushughulikia mwenyewe.


Rais anapoteua watu wa kumsaidia maana yake ni kumfanya yeye ashughulikie ishu kubwa za kitaifa na kimataifa ili taifa liweze kusonga mbele, badala ya kurudi nyuma na kushughulikia mambo madogo ambayo yangefanywa na wasaidizi wake.

Wananchi, fursa hii iliyotengwa na Rais ni muhimu kwenu kuitumia vizuri ili kero zenu zote ziweze kushughulikiwa ipasavyo.

Ni fursa ambayo itawafanya hata wale viongozi waliokuwa wamejisahau kuamka na kufanyakazi inayowapasa kwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Tuntule Swebe

## Muungwana Lazima Nilonge

# Komesheni matapeli simu, wasafisha nyota

**KATIKA** zama hizi za sayansi na teknolojia kuna furaha maana hakuna tena kugharamia stempu, bahasha wala karatasi ili kuandika barua.

Badala yake ni simu za mkononi. Ni kucheza nazo kuanzia ujumbe au sms, wasap, kuchati, kutuma picha na video yote hayo ni ili kuwasiliana.

Mambo hayaiishi hapo zama hizo watu walituma fedha vijijini kwa mabasi au kwa njia ya posta lakini wakati mwingine hazikufika.

Leo kuna simu, unatuma na mpokeaji anazipata papo hapo. Ni jambo jema la maendeleo ambalo limebadilisha maisha mijini na vijijini.

Hivyo ni suala ambalo hakuna anayelilalamikia linalorahisisha mawasiliano na kuongeza ufanisi kwenye karibu sekta zote.

Lakini kuna 'wabaya' wanaovuruga mambo wakifanya utapeli na matumizi yasiyofaa kwenye anga la mawasiliano wakitumia simu.

Wanafanya vitu visivyo vya halali wapo wanaopiga simu na kujifanya ni wahudumu wa kampuni za simu na wanataka kumpa mteja huduma ambayo si kingine bali ni kumlaghai.

Wanatumia mambo mengine kwa wakati tofauti. Muda mwingine wanawadanganya kuwa wameshinda bahati nasibu hivyo watume kiasi fulani cha fedha ili kuanzisha mchakato wa kuwapatia fedha zao.

Pamoja na hayo, wanadanganywa kuwa kuna wateja wamekosea kutuma pesa zikaingia kwenye simu zao, hivyo wanatakiwa kuzirudisha.

Wakishapewa ujumbe huo wanapewa maelekezo zaidi ya kuchukua hatua za kurejesha muamala, lakini lengo la watu hao ni kuwahadaa na kuwaibia wateja.

Ni jambo ambalo kila wakati linatokea na linazidi kukera licha ya kwamba simu kadi zimesajiliwa tena ikielezwa kwa kutumia alama za vidole na vitambulisho vya taifa.

Watu hawa wana lugha ya uongo na udanganyifu na wakati mwingine wanaweza kusema kuwa wanalenga kumsaidia mteja.

Ni zama za kukomesha na kupata dawa ya kukomesha utapeli huu. Ufanyike utafiti na kuujua ukweli wa wizi huo kwa sababu wanaohadaa wanaongezeka na wateja wanapata ujumbe wa aina mbalimbali.

Ujumbe unaowafukia ni mwingi kuanzia kujiunga na freemason, kupata tiba kwa waganga, kushind a bahati nasibu na kukosea muamala.

Wazazi na walezi nao wanahadaiwa kuwa watoto shuleni ni wagonjwa au wako hospitalini, ujumbe unataka watume fedha na tena kwa haraka.

Ukweli ni kwamba watu wamechoka ndiyo maana wanawaomba polisi wanaoshughulikia uhalifu mitandaoni kufanyakazi na kuondoa shida hiyo.

Lakini, mbali na wizi wa mtandaoni pia kuna waganga wa kienyeji kwani miongoni mwao wanaamini kuwa watu wana shida mbalimbali za kifamilia na wengine wanasumbuliwa na magonjwa na ndipo utapeli wa waganga unapojiri.

Waganga hao wanajidai kuwa wanaweza kusafisha nyota na kuongeza kipato, kuwafanya wenye kesi kushinda, kuongeza mvuto kwa wanawake, biashara na uwekezaji kukua na kama una madeni yakasahaulika, yote hayo yakifanywa kupitia mtandao wa matapeli.

Waganga hawa wanalenga kuiba mali za watu kuanzia simu, bidhaa na hata mali kama ardhi na mifugo.

Ikumbukwe Watanzania wengi hawana maarifa ya kung'amua hadaa hizo, hivyo huibiwa, kupata hasara na hata maendeleo ya wengi kurudi nyuma kwa sababu ya uovu huo.

Wapo watu wamepoteza pesa ambazo ni tegemeo, ada za shule zimechukuliwa kijanja na wakati mwingine, pesa za matibabu ya mgonjwa, za chakula cha familia na hata za miradi ya maendeleo, zote zikiangukia mikononi mwa waganga matapeli na hata watoa huduma za simu.

Tatizo hili linakua na linaendelea kuumiza watu, ndiyo maana kuna umuhimu wa kuchukua hatua na kuepusha mambo hayo.

Taifa likiacha wezi waendelee kushamiri ni wazi kuwa iko siku jamii itachukua hatua kama ambavyo imefika wakati wezi wakikamatwa wanachoma au kuumizwa mno.

Si vyema kumwaga damu za watu. Serikali ichukue hatua kwani watu wanajiuliza inashindwa nini?

## Ridhiwani: Wazazi tusaidie vita dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MBUNGE wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete amewataka wazazi kuhimiza maadili mema kwa familia zao, akiamini ndio njia sahihi kuisaidia serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Ridhiwani alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Vigwaza, Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo, akisema wazazi wanapaswa kusimamia maadili ya watoto wao.

Alisema wazazi wanapaswa kuzingatia misingi waliyolelewa nayo kwa kuirithisha kwa watoto wao ili wakue katika maadili mema.

"Kwenye maeneo yetu tuna maadili ambayo tumekuwa nayo, ukiyazingatia hakuna kitu kibaya kitakachotokea, tuwalee watoto wetu katika maadili mema, tuwakinge na kunyanyasika," alisema.

Mbunge huyo pia aliwataka walimu kufundisha wanafunzi shuleni kwa kuwapatia maarifa ya namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Pia aliahidi kuunga mkono majukwaa ya wanawake ili yaanzishwe katika maeneo mengi ya jimbo hilo na kuwa sehemu ya wanawake kukutana na kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Halmashauri ya Chalinze, Tatu Mpogo alisisitiza wanawake kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa kuwa tayari kuna soko la bidhaa.

# Boti ya uvuvi yazama siku nne baada ya kusajiliwa

**Na Maulid Mmbaga**

BOTI ya uvuvi ya MV Legacy yenye namba za usajili DS/L1175 inayomilikiwa na Yakoub Khamis, imezama ikiwa katika majaribio ya kufanya uvuvi pembezoni mwa fukwe za Bahari ya Hindi ikiwa ni siku nne tangu ipatiwe cheti cha usajili na ubora.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), boti hiyo ina urefu wa mita 11 na upana wa mita 1.7 na ilipatiwa cheti cha usajili na ubora Machi 6, mwaka huu ili kuendesha shughuli za uvuvi baharini.

Taarifa ilibainisha kuwa Machi 10, mwaka huu, saa 10:01 alasiri, Kituo cha Kuratibu Shughuli za Utafutaji na Uokoaji (MRCC) kilipokea taarifa ya kuzama boti hiyo, tukio lililotokea saa 9:50 alasiri karibu na ufukwe wa Coco, Msasani jijini Dar es Salaam, ikiwa na wavuvi sita, manahodha wawili na mhandisi mitambo.

"Kituo cha MRCC kilifanya jukumu lake la kisheria la kuratibu shughuli ya uokoaji kwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi Wanamaji na Zimamoto na Uokoaji na kufanya juhudi za kufika eneo la tukio na kuendesha zoezi la uokoaji.

"Watu wote tisa wamefanikiwa kuokolewa na wanaendelea vizuri kiafya bila ya kuwa na changamoto yoyote," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Pia ilielezwa kuwa boti hiyo ambayo ilikuwa katika majaribio ya kiufundi baada ya matengenezo ya mifumo ya uvuaji samaki, ilianza majaribio saa tatu asubuhi siku ya tukio ikitokea Tandavamba, Kivukoni na kufanya majaribio ya kuvua samaki wakizunguka maeneo yenye maji mafupi karibu na Daraja la Tanzanite Upanga hadi Coco Beach.

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa ilipofika saa 9:50 alasiri wakati nahodha anabadilisha uelekeo wa boti kuelekea upande wa kulia ndipo kamba moja ya upande wa kushoto ilipokatika na kusababisha uzito kuelemea kwenye kamba ya upande wa kulia ndipo uzito ulipohama ghafla na kusababisha boti kujaa maji na kuzama.

"TASAC inaendelea kutoa rai kwa wamiliki na waendeshaji vyombo majini kuzingatia sheria na kanuni za udhibiti usafiri majini na kuhakikisha muda wote wanavaa majaketi okozi ili kujiepusha na maafa yanayoweza kusababishwa na tukio la ajali," shirika hilo lilieleza katika taarifa hiyo.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akikabidhi tuzo kwa Ofisa wa Sheria wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Elizabeth Karua, kutambua mchango wa kampuni hiyo kudhamini Jukwaa la Kuinua Wanawake lililofanya mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamwahidi Samia kuwezesha wanawake katika sekta madini

**Na Mary Geofrey**

ANGLOGOLD Ashanti, kampuni mama ya Geita Gold Mining Limited imemwahidi Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kuwa sehemu ya mabadiliko chanya ya ushiriki wa wanawake na usawa wa kijinsi mahala pa kazi katika biashara na uhusiano wa wafanyakazi wao.

Ni ahadi iliyotolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ubia na ushirika Afrika, Simon Shayo alipohutubia maadhimisho ya Jukwaa la Kuinua Wanawake.

Jukwaa hilo lilifanyika sambamba na kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, likichagizwa na kaulimbiu ya 'Wekeza kwa Wanawake, Ongeza Kasi ya Maendeleo'.

Shayo alitoa rai kwa wadau na kampuni nyingine kuungana na Rais Samia aliyekuwa mgeni rasmi katika jukwaa hilo kuitoa Tanzania mahala ilipo na kuwa nchi ambayo itapigiwa mfano katika suala la usawa wa kijinsia.

"Tunakushukuru kwa kuendelea kuonesha njia, tunaishukuru sana serikali kwa kuonesha kwa makusudi namna ambavyo wanawake wanaweza kushiriki kwenye nafasi za uongozi, hii tumeiona kwenye baraza la mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, taasisi na vyombo vya ulinzi na usalama," alisema.

Alisema Canada ambayo ndio moja ya vinara katika uchimbaji madini, ina asilimia 16 ya wanawake katika sekta ya madini, hivyo Tanzania imepiga hatua kupitia majukwaa hayo pamoja na juhudi wanazofanya za ushiriki zaidi wa wanawake katika sekta ya madini.

"Katika Kampuni ya AngloGold Ashanti, Mwenyekiti wa Bodi ni mwanamke, lakini viongozi watatu kati ya viongozi wakuu saba ni wanawake, tena nyadhifa za muhimu kama Ofisa Mkuu wa Fedha, Ofisa Mkuu wa Sheria na Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu," alisema.

Alisema GGML pia haipo nyuma katika ushiriki wa wanawake kwenye uchimbaji kwa kuwa inao kwa asilimia 13.

"Tunajikongoja lakini tupo karibu sana nchi ambazo zimepiga hatua kwenye uchimbaji. Tunayo malengo ya kuhakikisha kuna ushiriki wa wanawake ambao si kwenye nafasi za usaidizi bali hata ambazo wanaume wanashiriki.

"Tumehakikisha tunaleta wanafunzi kwenye uanagenzi na walau kukaa nao mwaka mmoja na tunahakikisha asilimia 50 ni wanawake, pia kwenye sera ya ajira tunapofanya upembuzi wa walioomba kazi lazima asilimia 50 iwe wanawake na wanapofungana mwanamume na mwanamke kwenye usaili tunamchukua mwanamke," alisema.

Aliongeza kuwa katika miaka minne hapakuwa na nafasi za wanawake kwenye uongozi na sasa kupitia programu ya Female Future Tanzania inayoendeshwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), wamefanikiwa kuwa wanawake wawili kwenye nafasi za menejimenti.

Katika maadhimisho hayo ya Siku ya Wanawake Duniani, Rais Samia alitoa rai kwa wanawake kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Ninapenda kuhamasisha wanawake wenzangu kushiriki katika uchaguzi huu kwani wakifanikiwa kushinda katika nafasi zao patakuwa mojawapo ya jukwaa la kuzungumza na kutatua changamoto zinazowakabili wanawake," alisema.

Alisema licha ya serikali yake kujitahidi kufikia usawa wa asilimia 50/50, malengo hayo hayawezi kufikiwa kirahisi bila kuwapo malengo ambayo yanakwenda sambamba na mwamko kutoka ndani ya jamii.

# Madereva wa kirikuu, boda, bajaji wavutana Kariakoo

**Na Maulid Mmbaga**

MVUTANO umeibuka kati ya madereva wa magari madogo maarufu kama kirikuu, taxi, bajaji na bodaboda wanaofanyakazi ya kubeba mizigo jambo linalowafanya wakose kazi.

Aidha, wamesema wao (kirikuu) wamesajiliwa kwa ajili ya kubeba mizigo na pikipiki na bajaji ni kwa ajili ya abiria, lakini kwa sasa wanabeba mizigo hali inayowafanya wakose wateja huku wanawajibika kulipa kodi mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana mmoja wa madereva hao, Arufani Adam, anayeegesha gari lake Gerezani, Kariakoo jijini Dar es Salaam, alisema waendesha pikipiki wanabeba hadi mbao, magodoro na vifaa mbalimbali hali inayowasababishia washindwe kufanya biashara katika eneo hilo.

Pia aliwatupia lawama waendesha bajaji kwa tabia ya kutofuata utaratibu wa maegesho hali inayosababisha kuwapo kwa msongamano barabarani, unaowafanya madereva wa kirikuu kushindwa kushusha mizigo kwa wakati madukani.

"Hii hali imekuwa ikitusababishia kero kwa kiasi kikubwa katika eneo hili, kwa sababu kufuata utaratibu imekuwa ni tatizo kwao, lakini ile mizigo ambayo tulipaswa kubeba sisi pia wanakimbilia kuibeba wao kwa bei ya chini, tunataka waondolewe wakapaki eneo lingine wasichangamane na sisi," alisema Adam.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema kuna changamoto nyingi wanazopokea kutoka kwa watu mbalimbali na zinatatuliwa kwa kadri ya mazingira husika ili kutenda haki kwa kila upande.

Aidha, alisema serikali itahakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wasafirishaji hao wa Kariakoo ili kuhakikisha wote wanafanya shughuli zao kwa usawa na kutegemeana, na kwamba kero zote zitatatuliwa kwa kutumia njia ya maridhiano ili kila mmoja ajipatie kipato na aweza kujikwamua kimaisha.

"Sisi tunaishi kwa kutegemeana na nyinyi wote ni wafanyabiashara, kuna maofisa usafirishaji, madereva bodaboda, bajaji, tax, kirikuu na wafanyabiashara wa kwenye fremu bila kuwasahau wakazi wa maeneo hayo, sasa kila mmoja akimlalamikia mwenzake kuwa huyu haitajiki atolewe hili halijakaa sawa. "Wote mnategemeana, wewe mfanyabiashara wa kwenye fremu utamuhitaji bodaboda akukimbizie mzigo haraka sehumu fulani, mfanyabiashara pia utahitaji kirikuu ije ikuletee bidhaa hapo dukani kwako, vivyo hivyo kwa kila mmoja ndiyo maana tunasema wote mnategemeana isipokuwa ipo haja ya sisi kama serikali ngazi ya wilaya kukaa na wawakilishi wenu na kuangalia njia ya kuwapanga kila kundi kwa nafasi yake ili kila mmoja ajipatie riziki kwa nafasi yake," alisema Mpogolo.

Mbunge wa Ilala, Mussa Zungu, ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, aliwataka wafanyabiashara na madereva wa Kariakoo, kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya kufanyia biashara, huku akiwasisitiza kuboresha huduma katika biashara zao, ili kuendelea kuwavutia wateja wao.

"Ni lazima na nyie mtambue kile mnachokifanya, jitahidini kuboresha mazingira yenu ya ufanyaji biashara kwani vipo vitu vingi vinavyoweza mvutia mteja kuja kupata huduma kwako, kama una duka basi weka hata maji kama zawadi ya mteja pindi anapokuwa dukani kwako akipata huduma," alisema na kuongeza:

"Kama ni dereva basi uwe na lugha nzuri kwa abiria wako ikiwezekana msaidie kumfunga hata mkanda, hiyo ndiyo njia nzuri katika ushindani wa kibiashara," alisema Zungu.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (katikati), akizungumza na viongozi wa CCM wa Halmashauri Kuu wa kata hiyo walipokagua ukarabati wa madarasa katika Shule ya Bunge jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NEEC kuandaa mtaala kujifunza ujasiriamali shule za msingi nchini

**Na Christina Mwakangale**

WIZARA ya Elimu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), wanatarajia kuandaa mtaala kwa shule za msingi, maalum kwa mafunzo yanayohusu ujasiriamali, kwa lengo la kukuza tija katika mfumo wa kujiajiri.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, Maonyesho ya Wanawake Wajasiriamali 2024', yaliyofanyika katika viwanja vya ubalozi huo, kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, kila mwaka.

Alisema Tanzania ina takribani wajasiriamali milioni tano, miongoni mwao wanawake ni asilimia 54 ambao wamo katika biashara ndogo na kati, wakiwamo wanaokumbwa na vikwazo vya upatikanaji mitaji.

"Wanawake hawa wanakumbwa na changamoto za elimu duni kwenye teknolojia kuhusianisha na biashara zao hasa kinamama watu wazima. Kati ya wajasiriamali hao ni asilimia 16 pekee ndio wapo kwenye uwezekano wa kukopesheka," alisema Beng'i Issa.

Alisema baraza hilo lina mkakati endelevu nchini, kutoa elimu kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi, ili watakapojiajiri baadaye watambue mbinu za ujasiriamali, ikiwamo kupata masoko na kujenga mtandao kati ya kundi moja na lingine ndani na nje ya nchi.

"Tunawahimiza wanawake hawa kujiunga kwenye majukwaa ambayo ni rahisi kuwafikia. Tayari kuna majukwaa 4,000 ya kiuchumi ambayo yanaleta mwamvuli wa pamoja," aliongeza.

Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri, alisema katika maonyesho hayo ni takribani wanawake 50 wamefika kuonesha shughuli zao na mikono zinazowaingizia kipato na kukuza uchumi wa taifa.

"Siku ya wanawake ni kila siku, sio hadi ifike Machi 8, kwa mwaka mara moja. Lengo ni kufurahia juhudi za wanawake katika maendeleo ya jamii. Tuinue sauti zao kwa kuwaunga mkono. Ndio sababu Morocco kila mwaka huandaa tukio hili," alisema Balozi Zakaria.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoul, alisema katika kila mradi unaotekelezwa Tanzania na Afrika, ni lazima uwe na usawa wa kijinsia na wanawake ni kundi muhimu linalohitaji kuungwa mkono.

"Tunafanya kazi na wanawake katika miradi ya kilimo, biashara, ubunifu, sanaa, miezi michache ijayo tutajikita katika upikaji salama. Tunajua thamani ya mwanamke ndio maana wiki iliyopita Ufaransa imepitisha haki ya kikatiba kwao kuruhusu utoaji mimba," alisema.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) Mercy Sila, alisema kwamba wanawake wana mchango mkubwa katika uchumi na pia kuondolewa na vikwazo miongoni mwao kutaimarisha ujenzi wa shughuli za uzalishaji.

## 'Ujuzi rasilimali watu kigezo cha uzalishaji wenye tija'

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Mohammed Besta, amesema rasilimali watu ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi katika nchi yoyote na inahitaji kujengewa uwezo, hasa kwenye eneo la ujuzi na maarifa.

Mhandisi Besta anaunga mkono mikakati ya serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuinua makandarasi wazawa nchini kwa kuwajengea uwezo na uzoefu kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo ujuzi wa kitaalamu na maarifa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mhandisi Besta alisema kuna uhusiano mkubwa kati ya uwezo wa kiutendaji wa rasilimali watu iliyopo katika taifa, unaojumuisha ujuzi, maarifa na uzalishaji wenye tija.

Alisema nchi au taifa lolote likitaka kufikia maendeleo ya kiuchumi, lazima lijali, litunze na kuiendeleza rasilimali watu iliyonayo hasa kwa kuwekeza katika eneo la ujenzi wa ujuzi na maarifa yake.

"Ujenzi wa uwezo katika ujuzi na maarifa ya rasilimali watu haupaswi kubagua taaluma, kwa sababu uchumi wa nchi unajengwa na watenda kazi kutoka katika fani (taaluma) nyingi tofauti na wala haujengwi na fani moja.

Kwa mujibu wa Mhandisi Besta, utaratibu uliopo sasa wa kujali na kuthamini sana ufaulu katika taaluma unapaswa kuzungumzwa upya, ili kuchochea mabadiliko.

Alisema, Tanzania kama ilivyo mahali kwingine Afrika, imekumbwa na tatizo la baadhi ya watu wake kukosa ujuzi na maarifa katika mambo kadhaa na kutofikia viwango vya uzalishaji wenye tija vinavyotakiwa.

Aidha, alisema taifa lolote likitaka kuyafikia maendeleo ya kiuchumi yaliyo kusudiwa ni lazima lijitafakari kuona kama lina mikakati yoyote ya kukuza uwezo wa rasilimali yake katika eneo la ujuzi na maarifa.

"Ikiwa mikakati hiyo haipo ni vyema ikaandaliwa programu na miundo itakayosapoti kuendelezwa au kujengewa uwezo kwa rasilimali watu," alisema.

**Alisema nchi au taifa lolote likitaka kufikia maendeleo ya kiuchumi, lazima lijali, litunze na kuiendeleza rasilimali watu**





## RC Mongela aagiza watuhumiwa wa uhujumu uchumi wahojiwe

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ameagiza kuhojiwa kwa baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, ambao wanadaiwa kuhusika kuhujumu ukusanyaji wa mapato.

Aidha, amemtaka Mkuu wa wilaya hiyo, Felician Mtahengerwa, kuwachukulia hatua kali za kisheria watumishi hao baada ya kuhojiwa na mamlaka husika.

Mongela, ameagiza hayo kupitia kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa huo (RCC), baada ya hujuma hizo kuripotiwa.

"Kumeibuka hoja kuhusu baadhi ya watendaji, hasa wa Halmashauri ya Jiji la Arusha kuhujumu ukusanyaji wa mapato. Nikiwa kama mwenyekiti wa kikao hiki, natoa maelekezo kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, kuhakikisha anawachukulia hatua wahusika wote, ambao wameonekana kufanya ujanja ujanja katika ukusanyaji wa mapato," alisema.

Kutokana na madai hayo, amewaonya watumishi wa umma kwenye halmashauri za mkoa huo wanaojaribu kuhujumu ukusanyaji wa mapato, watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo, alisema baada ya kufika wilayani hapo, akitokea Wilaya ya Misenyi, alikutana na changamoto ya kusuasua kwa ukusanyaji wa mapato.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema katika Jiji la Arusha, kuna watumishi ambao sio waadilifu na wamekuwa kikwazo cha kusuasua kwa ukusanyaji wa mapato.

Alisema baada ya kubaini jambo hilo kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, walianzisha mpango mkakati wa kukusanya mapato na ndani ya wiki moja walifanikiwa kukusanya Sh. milioni 500.

# Kliniki ya TANESCO nchini yapunguza malalamiko

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KLINIKI ya Shirika la Ugavi Umeme Nchini (TANESCO), inayolenga kuboresha mfumo wa utoaji huduma kwa wateja wake ili kupunguza malalamiko, imeanza kutatua tatizo la wananchi waliokuwa wakisotea huduma ya kuunganisha umeme, tangu mwaka 2021.

Jana Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Kilimanjaro, Dotto Chacha, akizungumza na wakazi wa Kata ya Kibosho Kati, Wilaya ya Moshi, alisema kliniki hiyo pamoja na mambo mengine inalenga kusogeza huduma hiyo karibu na wateja, kupunguza wizi wa umeme na vishoka.

"Kwa siku moja, tumetatua malalamiko 124 katika Kata ya Kibosho Kati, kama sehemu ya utaratibu wetu mpya wa utatuzi wa kero za wateja kata kwa kata. Sisi Kilimanjaro, tuna kauli mbiu yetu 'TANESCO Kilimanjaro fahari ya mteja'. Hivyo ni lazima tumfuate mteja na kutatua malalamiko yake ili waendelee na shughuli za maendeleo.

"Tuwameona wateja 124, wateja 42 ni wanaume na wateja 82 ni wanawake. Hii inaonyesha ni jinsi gani wanawake wanahangaika na shughuli nyingi, ambapo tukiendelea hivyo tutaweza kuwasaidia kupunguza gharama," alisema Chacha.

...Lakini pia, tumetoa huduma za maunganisho ya awali, watu 12 wameomba leo na kuunganishiwa umeme, wapo wateja 22 walikuwa na matatizo ya mita, ambazo zote tumewatatulia."

Katika kliniki hiyo, Fundi Mkuu wa TANESCO Kilimanjaro, Peter Kulwa, alisema wamebaini kuwapo wateja wengi ambao tayari wamepeleka maombi tangu 2021, ila hawajaunganishiwa umeme na wengine hupata uvivu wa kufika ofisini kutokana na gharama ya usafiri.

"Kutoka hapa tulipo Kibosho Kati, hadi ofsi yetu ya mkoa ni zaidi ya kilomita 20. Kwa hiyo wateja wengi walishindwa kufika na wengine kubanwa na shughuli za hapa na pale.

Diwani wa Kibosho Kati, Bahati Mamboma, alisema ana kila sababu ya kuwataka TANESCO kuendelea na kliniki hiyo katika siku zijazo, kwa sababu katika kata yake zaidi ya wananchi 150 wamesikilizwa na 70 wamewashiwa umeme.

"Kitongoji cha Ngoroshi hatukuwahi kuwa na umeme lakini leo tumepewa uhakika baada ya nguzo kwenda kumwagwa pale na kuanza kusimamishwa, tunaomba kuharakisha ili kuwasaidia wanafunzi kuweza kufanya vyema katika masomo yao na kuongeza usalama nyakati za usiku," alisema Frida Kimati.

Aidha, katika Baraza la Madiwani la robo ya pili ya mwaka, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Moris Makoi, waliiomba shirika hilo, kutatua matatizo ya umeme katika vijiji hasa wizi wa mita, wananchi ambao hawajaunganishiwa umeme, nguzo mbovu na waya zilizopo nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kulia), akiwasiliana na viongozi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhusu kutatua changamoto ya wazee wa Kitongoji cha Kairo wenye umri zaidi ya miaka 70 kulipishwa kila mwezi fedha za kodi ya jengo kupitia malipo ya ankara ya nishati ya umeme (Luku) kwenye nyumba zao katika mkutano wa hadhara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbunge aumizwa wanaokopa mikopo umiza

**Na Godfrey Mushi,** HAI

IDADI ya wanawake wanaochukua mikopo ya kausha damu na taasisi ndogo zinazotoa huduma za fedha na kisha kushindwa kuilipa, inamuumiza kichwa, Mbunge wa Hai, mkoani Kilimanjaro, Saashisha Mafuwe.

Kutokana na tatizo hilo, Mafuwe, amesema ofisi yake imejikuta inabeba mzigo huo wa kuwalipia madeni yao wanawake ili kuepusha mali zao kuuzwa na kuziachа familia hazina kitu.

Alikuwa akizungumza juzi katika Kata ya Narumu, alipokwenda kuwaunga mkono, Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), waliokwenda kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani katika eneo hilo.


Kutokana na mwenendo huo, mbunge huyo, amewataka wanawake kuacha tabia ya kuchukua mikopo bila ya kuwa na mpangilio wa matumizi ya mikopo hiyo.

"Hivi sasa kumeibuka mtindo wa wanawake kuchukua mikopo hiyo bila sababu, huku wengine wakishindwa kuwashirikisha waume zao.

...Katika ofisi yangu nimepokea malalamiko kadhaa, huku wakati mwingine, nikilazimika kuwalipia baadhi yao ili kunusuru kuuzwa kwa mali zao. Jambo hili limekuwa likiwatia kwenye matatizo, ikiwamo kuuzwa kwa nyumba au kuchukuliwa kwa mali na taasisi za mikopo," alisisitiza Mafuwe.

Kuhusu mikopo ya asilimia 10 isiyo na riba, ambayo ilikuwa ikitolewa na halmashauri zote nchini, ameyataka makundi maalum yanayonufaika ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuwa na subira, kwa kuwa serikali itaanza kuitoa wakati wowote.

"Endeleeni ndugu zangu wanawake, kuwa wavumilivu kwa kuwa serikali ilizuia kutoa mikopo hiyo kwa muda ili kwenda kuandaa utaratibu mzuri utakaosaidia kuhakikisha kuwa kila kundi linapata na pia litarejesha kwa wakati," alieleza.





# Waislamu wakumbushwa kutenda wema wakati mfungo Ramadhani

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

WAUMINI wa dini ya kiislamu mkoani Mwanza wameungana na wenzao ulimwenguni kuanza mfungi wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, huku wakikumbushwa kuzingatia matendo mema.

Wito huo umetolewa na Imamu wa Msikiti wa Abbakari bin Zuberi, Shekhe Hanafi Shabani wakati wa kongamano la kuukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhani Mosi 1445H.

Alisema katika imani ya dini hiyo kufunga ni jambo la lazima kwa mujibu wa sheria.

Shekhe Hanafi alizitaja fadhila za kufunga kuwa ni pamoja na mwanadamu kupata msamaha kutoka kwa Mungu, kufuta dhambi ndogo, kuachwa huru na moto wa jahanamu, kuepuka adhabu Mungu.

"Mtume Muhammad (S.A.W) alisema kwa atakayefunga kwa imani na kutarajia malipo kwa Mwenyezi Mungu basi Mola wake atamsamehe madhambi yake yote yaliyo tangulia, hali ya kuwa mtu huyo hakurudia dhambi kubwa na kuzingatia matendo mema,"alisema Sheikh Hanafi.

Katika kongamano hilo lililofanyika wilayani Ilemela mkoani Mwanza lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa dini hiyo akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Johari Samizi.

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Johari Samizi aliwataka waamini hao hususani wanawake kuhakikisha wanafunga pasipo kuwa na visingizio kwani zipo hukumu za kutofunga kwa atakayeacha kufanya hivyo kwa makusudi.

"Hiki kipindi ndicho watu wengi huwa na sababu nyingi na udhuru za maradhi, ndio huwa zinaibuka kipindi hiki hivyo niwaombe msiwe watu wa namna hiyo badala yake tukumbushane katika kutimiza nguzo hii," alisema Samizi.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala alisema katika kipindi hiki cha mfungo wasisite kuwashirikisha katika jambo lolote kwani wao ni waumini pia wa dini ya kiislamu licha ya kuwa ni viongozi wa kiserikali.

Alisema: "Tunajiskia fahari kutushirikisha katika jambo hili kwa sababu tunajiona bado tupo na wenzetu, hivyo tumefarijika kwani wakati mwingine ni ngumu kujifanyia tathmini mwenyewe namna watu wanavyo kuchukulia."

# Polisi yasisitizwa kutunza siri za watoa taarifa

**Na Benny Kingson,** TABORA

ASKARI wa Jeshi la Polisi mkoani Tabora wametakiwa kuwa waadilifu kazini kwa kuhakikisha wanawalinda na kutunza taarifa za siri za watoa taarifa za uhalifu.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zakaria Mwansasu alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwenye kilele cha siku ya familia ya polisi.

Alisema kuwa watoa taarifa wanapaswa kulindwa na taarifa zao hazitakiwi kuvujishwa kwa usalama wao.

Mwansasu alisema kumekuwapo na malalamiko ya wadau kudai baadhi ya askari wa jeshi hilo kutokuwa waaminifu kwa kukiuka maadili ya kazi zao, kwamba wamekuwa wakitoa siri za taaarifa wanazopewa na wananchi kuhusu wahalifu.

"Unakuta raia mwema ametoa taarifa za matukio ya uhalifu na kuwataja walengwa, baadhi yenu wamekuwa wakivujisha taarifa hizo na kupelekea watoa taarifa kuingia matatani. Pia inawavunja moyo wa kuendelea kuwapa taarifa muhimu, tubadilike na kuacha tabia hii," alisema Mwansasu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, SACP Richard Abwao, alisema wiki hiyo ya familia ya polisi wamefanya ukaguzi katika wilaya zote nane za mkoa huo kuona ufanisi na changamoto zilizopo na ufumbuzi wa haraka kuhakikisha hazirudii mara kwa mara.

Alisema mwaka 2022 katika kipindi cha Januari hadi Desemba kulipatikana na matukio 16,169 na hadi mwaka 2023 yameripotiwa matukio 16,553 ikiwa ni ongezeko la matukio 384 sawa na asilimia 2.4, kwamba wanaendelea kupambana kuhakikisha hali ya amani inaongezeka mkoani hapa.

Kuhusu matukio ya jinai SACP Abwao alisema mwaka 2022 yalikuwa 2,212 na mwaka 2023 yalikuwa 1,902 ikiwa ni pungufu ya matukio 110 sawa na asilimia 5.5.

Alisema katika matukio ya usalama barabarani mwaka 2022 yalikuwa 52,484 na mwaka 2023 matukio 63,965 ikiwa ni ongezeko la matukio 11,482 sawa na asilimia 21.9.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora, Ramadhani Kapela, aliwataka baadhi ya askari wa jeshi hilo kuacha kutumia nguvu na kuwatisha wananchi.



Mbunge wa Butiama ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, akisimikwa na wazee wa jadi wa Bukwaya, Kata Bisumwa, mkoani Mara kuwa rafiki wa amani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waliovamia hifadhi ya barabara Shinyanga wapewa salamu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga waliovamia hifadhi ya barabara kwa kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo, wametakiwa kuondoka kabla ya kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Kaimu Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Samweli Mwambungu, wakati akielezea mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Samia madarakani.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakivamia hifadhi za barabara na kufanya shughuli mbalimbali za kibinadamu kikiwamo kilimo na kuziharibu, hali ambayo inasababisha kutumika kwa fedha nyingi katika matengenezo.

Alisema kutokana na uharibifu huo tayari wameshaandaa mpango mkakati wa kuwaondoa wananchi wote ambao wamevamia hifadhi ya barabara, huku akiwasihi kuanza kuondoka kwa hiari yao wenyewe kabla ya kuanza kuondolewa kwa nguvu.

"Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 Kifungu Namba 13 kinasema mwananchi anapaswa awe umbali wa mita 30 kutoka kwenye hifadhi ya barabara, ili panapo hitajika kufanya upanuzi wa barabara kusiwe na usumbufu," alisema mhandisi Mwambungu.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu wamepokea Sh.bilioni 47.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yakiwamo matengenezo ya barabara.

Pia alitaja miradi ya kimkakati ambayo wanaitekeleza, kuwa ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 50.3 kutoka Mwigumbi- Lamadi kwa gharama ya Sh. bilioni 72.2, Kagongwa- Bukoba hadi Nzenga Kilomita 66, Kahama- Kakola Kilomita 73 kwa gharama Dola za Marekani milioni 40.

Alisema pia upo upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli katika Manispaa ya Shinyanga wenye gharama Sh.bilioni 49 na ujenzi wake upo asilimia 10.51.

Alisema upanuzi wa uwanja huo umetoa ajira kwa wazawa 86 na raia wa kigeni 15 tu, kwamba ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu.

Alisema kazi nyingine ni uwekaji taa za barabarani 395 kwa gharama ya Sh.bilioni 1.18, na kubainisha kuwa kwa sasa wapo kwenye utaratibu wa kuzifanyia marekebisho taa 180 ambazo zimepata hitilafu na nyingine kutowaka kabisa.



Ukurasa 12

**BOOST inavyosisimua elimu Korogwe, wanafunzi wamwahidi kitu Rais Samia**



Ukurasa 13

Mchawi wa mwanamke kwenye siasa ni kutokubalika

Nipashe

# TESA

Jumanne Machi 12, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**JKCI inahitaji eneo kubwa kupanua na kutoa huduma**

ELIMU

NA SHABAN NJIA, KAHAMA

# Askari UNFPA, WiLDAF wanavyoongeza nguvu vita ukeketaji Shinyanga na Mara

BAADHI ya makabila huamini kuwa ukeketaji ni mila 'bora' kwa madai kuwa inadhibiti mihemko ya kimwili na kuzuia wanawake kwenye ndoa kuchepuka.

Aidha, wapo wanawake na wanaume wakubwa kwa wadogo wanaoitetea hoja hiyo wakidai kuwa waliokeketwa hawawezi kuchepuka, ni waaminifu, hata wasichana ni watulivu na wasioshiriki kujamiiana wanaofaa kuoa.

Yote hayo yakaonekana ni kuendeleza mila kukandamizi na ukatili kwa wanawake, ndiyo maana ilipofika mwaka 1998 ikaandikwa historia, taifa lilipoanza kutumia sheria ya makosa ya kujamiiana iliyoharamisha ukeketaji watoto kuwa makosa la jinai.

Licha ya juhudi nyingi kufanyika ukeketaji na ukatili unaelezwa kuenea maradufu vijijini kwa asilimia 13 kuliko mijini ambako ni asilimia tano, hayo yakithibitishwa na takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) za mwaka 2018, kwamba ongezeko la wasichana walio katika hatari ya kukeketwa inaongezeka.

Utafiti wa Kidemografia na Afya (Tanzania Demographic and Health Survey) wa mwaka 2015/2016 unaonyesha mikoa yenye viwango vikubwa kwa utekeketaji na ukatili ikiwamo Manyara kwa asilimia 58, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41, Mara asilimia 32 na Singida asilimia 31.

Katika juhudi za kupambana na ukatili huo, serikali inaweka mpango wa taifa wa utekelezaji wa kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto (NPA-VAWC) 2017-2022), unaoeleza kuwa ukeketaji ni mila inayoathiri wanawake na watoto kama sehemu ya utekelezaji wa ajenda ya maendeleo endelevu ya 2030.



Wasichana waliosomea ususi wakifurahia vifaa vya kazi kutoka WiLDAF na UNFPA, walivyokabidhiwa ili kuendeleza ujuzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

Aidha, Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na UNFPA wamekuja na mradi wa "chaguo langu haki yangu" lengo likiwa kuwaelimisha wanawake na watoto kuhusu ukatili wa kijinsia na ukeketaji katika mikoa ya Shinyanga na Mara kwa msaada wa Finland.

Joyce Kessy, Mratibu Mradi wa chaguo langu haki yangu kutoka WiLDAF, anasema ukeketaji na ukatili wa kijinsia umejikita kwenye kanuni na taratibu za kijamii, imani za kiutamaduni na vichocheo vya kiuchumi na inachukuliwa kama jambo la muhimu katika shughuli za jando na unyago jambo ambalo sio kweli.

Anasema, kuanzia 2022 hadi sasa wamewafikia mabinti 1,073 wenye umri kati ya 15 hadi 25 wa mikoa hiyo na kuwapatia elimu ya afya ya uzazi, madhara ya mimba na ndoa za ututoni kwa lengo la kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukeketaji kwenye familia wanazotoka.

Anasema, kati ya hao, 610 ni wenye miaka 10 hadi 19 ambao ni kundi linalobalehe ambao wamepewa elimu ya stadi za maisha, afya ya uzazi na namna ya kujikinga na ukatili wa kijinsia na maambukizi ya VVU huku 463 wenye miaka 15 hadi 24 wakipewa ufadhili wa mafunzo ya vyuo vya ufundi (VETA).

Aidha, anasema wazazi na walezi wamekuwa na ushiriki mdogo kwa sababu wengi wao wanataka mabinti waolewe na kujipatia fedha au ng'ombe na wale wenye watoto wanaoishi na ulemavu wanawaficha bila kujua ni rahisi kufanyiwa ukatili wa kijinsia ikilinganishwa na wengine.

Joyce anasema licha ya kuwapatia elimu ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia, ukeketaji na ujuzi wa fani mbalimbali kulingana na kile wanachokihitaji, wanawapatia vifaa kazi ili kuendeleza walichojifunza na kujikwamua kiuchumi.

Anaeleza kuwa wamepewa vyerehani, vifaa vya saloon kama viosha na vikaushia nyweli (hair dryers) na vingine kulingana na fani walizosoma.

Mwaka huu wasichana 249 wamewafikia kati ya hao 84 wanatoka Manispaa ya Kahama, 76 Kishapu na 84 Butiama mkoani Mara, anasema Joyce akiongeza kuwa pia wapo wengine wanaoendelea na masomo katika vyuo vya VETA watakapohitimu watapewa ufadhili wa vifaa vya kazi.

Anafafanua kuwa wameingia makubaliano na mabinti, wazazi, walezi na ofisa maendeleo ya jamii ili kufanikisha kuwa wanavitumia vifaa hivyo kwenye matumizi yaliyopangwa na sio kuvikodisha kwa wengine, na wanaobainika wanachukuliwa hatua.

**WANUFAIKA**

Grace Julius (20) aliyepata ujauzito akiwa kidato cha pili na kuonekana hana maana mbele ya wanaomzunguka, anasema anatimiza ndoto zake kupitia fani ya ufundi umeme baada ya kupata msaada huo.

Mwingine Juliet Samwel(22), mkazi wa Butiama anasema, akiwa darasa la tano alikuwa afanyiwe ukeketaji hatua, iliyomfanya kukimbia nyumbani baada kupata hofu na kuacha masomo.


Anasema ameibuka tena akiwa mkubwa na vifaa vya ufundi alivyopata vitampa ajira na kumudu maisha yake.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA AUGUSTA NJOJI, KOROGWE

# BOOST inavyosisimua elimu Korogwe, wanafunzi wamwahidi kitu Rais Samia



Wanafunzi wakiwa katika mazingira mapya ya kujifunzia. **PICHA: BOOST**

UMBALI mrefu, utoro, uhaba wa miundombinu, msongamano madarasani ni miongoni mwa adha zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi wa shule mbalimbali za Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga.

Kupitia mradi wa uboreshaji elimu ya awali na msingi (BOOST) unaotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), adha hizo zinaelekea kuwa historia.

Ofisa Elimu Awali na Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Elias Mavua, anasema kabla ya mradi wa BOOST wanafunzi kukosa vyumba vya madarasa ilikuwa changamoto kubwa kwa halmashauri hiyo yenye wanafunzi 66,153.

"Baada ya kuletewa mradi wa BOOST mambo yamebadilika, yamekuwa mazuri, watoto wanakaa kwenye madarasa mazuri, wanasoma vizuri shida hiyo imeondoka kwa sehemu kubwa, nina imani tunavyoendelea, fedha zikiletwa changamoto hii itaisha," anasema.

Anafafanua kuwa katika mradi wa BOOST wamepata Sh. milioni 696.1 kwa ajili ya shule saba, mpya moja ambayo imegharimu milioni 348.5.

"Ujenzi wa shule hii umewaondolea adha wanafunzi aliokuwa wakitembelea kilomita 3.8 kutoka kwenye shule mama ya Makumba, hivyo watoto 273 wanasoma katika shule mpya kuanzia mwaka huu 2024," anasema.

George Mkelo ni Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Gereza iliyoko Kata ya Korogwe Vijijini, anasema kabla ya BOOST hawakuwa na darasa la elimu ya awali.

"Tulikuwa na darasa ambalo watoto wanasoma lakini lilikuwa halijakamilika, halina sakafu, watoto waliingia wakiwa wasafi lakini waliondoka wachafu kweli kweli mazingira hayo yalikuwa si salama sana kwa wanafunzi wanaoanza shule."

"Katika maeneo hayo hata utoro ulikuwa mkubwa kwani eneo likiwa halina ubora watoto kuja shule ni lazima umlazimishe, kujengwa kwa majengo haya yamechochea ufaulu," anasema Mkelo.

Anaeleza kuwa kwa sasa mahudhurio ya wanafunzi ni mazuri kutokana na uwepo wa mazingira bora ya kufundisha na kujifunzia.

"Tunaipongeza serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan anapambana kuhakikisha mazingira ya kusoma na kujifunza yanakuwa sehemu salama na kwa sababu kuna zile taratibu ambazo serikali inaweka kuhakikisha mtoto anasoma kuanzia shule ya awali mpaka kidato cha sita bila malipo. Sisi tunaona ameanza vizuri na ni faraja kwetu," anasema.

Mkuu wa Shule ya Msingi Makumba, Adinani Jumanne, anasema shule ina wanafunzi 805 kutokana na wingi wa wanafunzi na miundombinu iliyopo haitoshelezi, hivyo walipokea milioni 348.5 za mradi huo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule mpya yenye mkondo mmoja katika kitongoji cha Magunga.

"Changamoto iliyofanya sisi tupate shule hii ni wingi wa wanafunzi wanaotoka katika vitongoji vya Magunga, Mtemiroda na Mnazimmoja na changamoto ya mto uliokuwa unawazuia kutoka vitongoji hivyo," anasema Mkuu wa Shule.

Mwalimu Jumanne anasema, "Kipindi cha mvua wanafunzi kutoka kwenye vitongoji hivyo walikuwa wanapata changamoto ya kutokwenda shule kwa takribani mwezi," anafafanua Jumanne.

Anasema tatizo jingine ni utoro, kutokana na umbali wa zaidi ya kilomita 3.5 ambao watoto walikuwa wanatembea na kushindwa kuhudhuria shuleni.

"Ukiangalia watoro wengi walikuwa ni miongoni mwa vitongoji hivyo, kwa hiyo ilibidi tulitolee taarifa, tunaimani shule hii ikikamilika na kuanza kutumika itaokoa watoto hawa waliokuwa wanatembea kilometa nyingi kwenda na kurudi nyumbani," anasema.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Gereza, Rehema Kiyondo, anasema kabla ya mradi wa BOOST kulikuwa na mrundikano mkubwa wa wanafunzi katika darasa moja walikuwa karibu 120 kutokana na uhaba wa madarasa.

"Ufundishaji haukuwa na ufanisi wapo waliopata kile kinachofundishwa lakini wengine walimu walishindwa kuwafikia baada ya mradi huu tumekuwa na mgawanyiko wa madarasa," anasema.

Anabainisha kuwa fedha walizopokea kupitia mradi wa BOOST ni milioni 69.1 ambazo zitawezesha kujenga madarasa mawili, matundu ya vyoo sita na uzio unaozunguka madarasa ya awali.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Makumba, Michael Shemtagwa, anasema kukamilika kwa mradi huo kutanusuru watoto waliokuwa wanasombwa na maji kwenye mto hali iliyokuwa inahatarisha maisha yao.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mbeza Mazoezi Hilda Wiliam, anasema mradi wa BOOST umepunguza msongamano madarasani.

"Tunamwahidi Rais Samia kwamba tutasoma kwa bidii na kufaulu mtihani wa taifa na kupata alama za juu pia tutatuza vizuri madarasa kwa ustadi ili vizazi vijavyo viyatumie," anasema Hilda.

Ofisa Elimu Kata ya Manundu, Edna Kimonge, anasema: "Shule yetu kabla ya mradi wa BOOST ilikuwa na tatizo la upungufu wa madarasa kutokana na kuwa na wanafunzi wengi. Pia upungufu wa madawati na matundu ya vyoo ulikuwapo."

## Askari UNFPA, WiLDAF wanavyoongeza nguvu vita ukeketaji Shinyanga, Mara

**INATOKA UK.11**

Mmoja wa wazazi Zuwena Buhimbi, anasema, baadhi yao wamekuwa chanzo cha kukwamisha ndoto za watoto kielimu wakiwalazimisha waolewe licha ya kuwa bado ni wadogo kwa kutaka mahari, mifugo na fedha na kumlazimisha kufanya vibaya kwenye mitihani ya mwisho ya darasa la saba ama kidato cha nne ili wafeli na kuozwa.

Swaiba Chemchem Ofisa Ustawi wa Jamii Kahama anasema, mradi umewapati mwanga mabinti waliokosa matumaini hasa wale waliokatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali na sasa wanazitimiza kupitia njia nyingine na kuwata kujikita kwenye kujiwezesha kiuchumi ili kuondoka na kuingia kwenye vishawisha vya mapenzi tena.

Anasema, wameanzisha utaratibu wa kuwaunganisha kwenye vikundi vya ujasiriamali vilivyopo kwenye kata wanazotoka ili mikopo ya asilimia 10 ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu itakapoanza kutolewa basi wapate fedha hizo kama sehemu ya mitaji yao.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, anaahidi kuwapatia ajira za muda mabinti tisa kati ya 263 wenye ujuzi mbalimbali katika mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ili wajipatie fedha za mitaji na kuendeleza ujuzi waliopata.

Msumba anawataka wale wenye ujuzi mwingine kama ushonaji, kudarizi, mapambo, katibu muhutasi na upishi kutengeneza vikundi kwenye kata zao ili wawe na sifa ya kupata mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na halmashauri.

ELIMU
NA JENIFER GILLA

# Mchawi wa mwanamke kwenye siasa ni kutokubalika

MACHI ni mwezi wa wanawake, baada ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Ijumaa Machi 8, vuguvugu la kutaka usawa wa kijinsia na uwakilishi wa kiuwiano kwenye uongozi na taasisi za kisiasa kama Bunge na Baraza la Wawakilishi, linaendelea.

Lengo ni kutaka mwanamke apewe nafasi baada ya kufungwa kwenye minyororo ya mifumo kandamizi ndani ya jamii, ambayo haimkubali kuwa anamudu kuwa kiongozi na anaweza kufanya mabadiliko na kuleta mafanikio.

Maelezo anayoyatoa Rais Samia Suluhu Hassan, miaka mitatu iliyopita muda mfupi baada ya kuchukua uongozi wa taifa, ni kielelezo kuwa wanawake wanawahakikishia wanaowaongoza kuwa wanaweza, wanachohitaji ni kupewa nafasi.

Rais Samia alisema: "Aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini maumbile yake ni ya kike."

Anaeleza hayo kuwatoa wasiwasi Watanzania, hasa wale waliokuwa na hofu kuwa asingeweza kuivusha nchi katika kipindi kile kwa vile ni mwanamke, yaliyojiri baada ya hapo ni kuonyesha juhudi kuwathibitishia anaowaongoza kuwa mwanamke anaweza.

Tangu kushika madaraka miaka mitatu iliyopita na mambo makubwa aliyoyafanya katika nchi, yamebadilisha taswira kuhusu udhaifu wa mwanamke katika uongozi na kuwatia moyo wengi kuingia katika vinyang'anyiro vya siasa na uongozi.

Licha ya jitihada kubwa wanazofanya wanawake ili kushika nafasi mbalimbali za uongozi na kushiriki katika siasa bado safari yao imetawaliwa na milima na mabonde.

Idadi ya wanawake wanaotia nia ya kugombea nafasi mbalimbali kuanzia ngazi ya mtaa hadi kitaifa ni kubwa lakini wanaofanikiwa ni wachache.

Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), inasema kuna asilimia 2.1 ya wanawake wenyeviti wa vijiji, wakati asilimia 6.7 ni wenyeviti wa vitongoji pamoja na asilimia 12 ya wenyeviti wa mitaa, hiyo ikiwa idadi ndogo ikilinganishwa na namba ya vijiji na vitongoji vilivyopo nchini.



Vitoria Elangwa, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, akisherehekea Siku ya Wanawake Duniani na wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa Jangwani Sekondari. Anawahamasisha kuwa wanaweza hivyo waongeze bidii na uthubutu. **PICHA: TFRA**

Wakati bungeni kuna uwakilishi wa asilimia 37.4 na kwenye Viti Maalum ni asilimia 30 na pamoja na kuwa na wanawake wachache katika wizara muhimu.

Mkurugenzi LHRC, Anna Henga, anasema kuwa kuwapatia wanawake fursa katika uongozi kuanzia ngazi za chini kutafanikisha kuwasilisha ajenda zao, na taasisi yake imejipanga kuhakikisha wanapatikana viongozi wanawake katika serikali za mitaa.

Kufuatia hali hiyo wanawake viongozi na wadau wa maendeleo ya wanawake wanacharuka wakati midahalo mbalimbali juu ya yale yanayomrudisha nyuma mwanamke katika safari ya siasa katika Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani, Ijumaa wiki iliyopita.

Akiwa katika maadhimisho hayo Dodoma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema mtazamo uliojengeka katika jamii kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi unarudisha nyuma jitihada zake za kushika wadhifa huo pamoja juhudi kubwa anazofanya.

Anasema mtizamo huo husababisha mwanamke kukutana na vikwazo kuanzia ngazi ya familia ikiwamo kutopewa ushirikiano wa kutosha kwa ndugu na jamaa pale anapotangaza nia ya kuwania nafasi fulani.

Waziri Gwajima anashauri jamii iendelee kuelimishwa ili iondokane na dhana iliyojengeka miongoni mwa wengi kuwa wanawake hawastahili kuwa viongozi

"Wanawake jiungeni kwenye vikundi vya maendeleo ili mtumie fursa mbalimbali za uwezeshaji wa kiuchumi zinazotolewa na serikali na taasisi nyingine," anashauri Dk. Gwajima.

Aidha, anawashauri wanawake wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na kupiga kura simu ya uchaguzi.

> "Inawatia hamasa kuongeza ari na imani kuwa kutakupo na viongozi wengi wanawake miaka ijayo kama wakipewa msaada wanaouhitaji.

Wakili Fatma Karume, Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika, (TLS), anaeleza haja ya kuzitathmini upya sheria za uchaguzi kwa kuwa zimekuwa zikitoa nafasi chache kwa wanawake kuingia katika vyombo vya maamuzi suala linalowakwamisha juhudi za kuingia kwenye nafasi za uongozi na kufikia uwakilishi wa 50/50.

Mwenyekiti wa Bodi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Ananilea Nkya, anashauri nafasi za viti maalum kwa wanawake katika ubunge na udiwani ziondolewe ili wakachuane na wanaume majimboni.

Anasema viti maalum katika siasa vinachochea uunyanyasaji kwa wanawake, wanaume wakiwadharau na kuwaona kuwa ni daraja la pili, na hawana ubavu wa kusimama peke yao, jambo analolipinga.

"Tukiendelea kuving'ang'ania kutangaza kwamba hatutaki viondoke tunavihitaji maana yake tunatangaza kuwa wanawake hatupo tayari kwenda kufanya uwakilishi ulio sahihi na ambao ni wa uwajibikaji kwa wananchi," anasema.

Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, anasema uwepo wa rais mwanamke madarakani umeleta chachu kwa wanawake kutamani kuwa viongozi katika nyanja tofauti hali inayoleta matumanini.

Anaongeza kuwa inawatia hamasa kuongeza ari na imani kuwa kutakupo na viongozi wengi wanawake miaka ijayo kama wakipewa msaada wanaouhitaji.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari, Mwakilishi Mkazi Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN Women), Hodan Addo, anashauri serikali itekeleze makubaliano ya mikataba ya kimataifa inayoelekeza nchi wanachama kuchukua jitihada za makusudi za kisheria na kisera kufikia uwiano wa 50:50.

Ulinganifu wa kijinsia utawapa wanawake nafasi ya kushiriki katika utungwaji wa sera, sheria na utoaji uamuzi muhimu ambao unaathiri maisha yao katika ngazi ya jamii.

SAYANSI
NA DR. FELICIAN KILAHAMA


Huduma za upasuaji moyo zikiendelea JKCI. **PICHA: MTANDAO**

# JKCI inahitaji eneo kubwa kupanua na kutoa huduma

JINA la Hospitali ya Muhimbili, ni mashuhuri na pengine kila familia ina mtu anayelifahamu. Ni kutokana na umuhimu wake na kazi kubwa taasisi inayofanya inayomgusa karibu kila mmoja.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa ilianzishwa kati ya 1910 na 1920 chini ya utawala wa Wajerumani na Waingereza ikifahamika kama Hospitali ya Sewahaji.

Hata hivyo, mwaka 1956 Waingereza wakaibadilisha jina kuwa: "Princess Margret Hospital" na mwaka 1961 baada ya uhuru, ikaitwa 'Hospitali ya Muhimbili' hadi ilipotimia 1976 ilipoitwa Shirika la Afya Muhimbili, au Muhimbili Medical Center, ikifupishwa MMC.

Kadhalika, mageuzi yaliendelea hadi kuifanya 'Hospitali ya Taifa mwaka 2000. Kupitia utaratibu huo wa kisheria, taasisi mbili zilizaliwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Kishiriki Muhimbili (MUCHAS).

Hata hivyo, Novemba 2004 MUCHAS ikageuzwa kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS). Muhimbili inafanyakazi ikiwa ni Hospitali Kuu ya Taifa ya Rufani inayohudumia Watanzania na wagonjwa wengine kutoka mataifa jirani wanaokuja kutibiwa.

Moja ya watoa huduma kwa wagonjwa wa nje ya nchi, ni Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI). Ni miongoni mwa maendeleo yaliyofikiwa katika mabadiliko yaliyofanywa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi pia kinafanya tafiti za tibaasilia na mfanikio mengine makubwa ni kuwepo na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) ambayo ni chombo muhimu katika kuokoa maisha ya wagonjwa wengi wa mifupi na mifumo ya fahamu. Nikikumbuka tangu 2016 nilipofika JKCI mara ya kwanza na kulinganisha na hali ya sasa 2024, nashuhudia yamekuwapo maendeleo makubwa.

Shukrani kwa serikali kuanzisha JKCI kwa msaada wa fedha na utaalamu kutoka Serikali ya Japan, kadhalika, naishukuru serikali, kwa kuweka Sera na Taratibu za Bima ya Afya ambazo zinafanikisha wengi kufikia matibabu japo haijasambaa nchi nzima.

Upatikanaji wa huduma za afya kwa gharama nafuu na zinazotabirika na kuwa sawa nchi nzima, ni changamoto kubwa kwa walio wengi.

Ikumbukwe kupitia bima ya afya, inawezekana kwa wananchi wengi kuhudumiwa ipasavyo. Itakuwa vyema iwapo Watanzania wengi wataelewa umuhimu wa bima ya afya kwa maisha yao na kuchukua hatua za haraka kujiunga na huduma hii muhimu.

> "Kimsingi mtu anapaswa kuchangia gharama kwa kujiunga na huduma ya bima ya afya hata kama ni mzima kwa angalizo la kesho au miaka ya mbeleni.

Huduma za afya ni gharama kubwa sana hivyo ni vigumu kwa wengi kuzimudi bila bima ya afya, hivyo, kupitia utaratibu huo wengi wataweza kutibiwa ikiwa ni pamoja na matibabu ya magonjwa ya moyo.

Kimsingi mtu anapaswa kuchangia gharama kwa kujiunga na huduma ya bima ya afya hata kama ni mzima kwa angalizo la kesho au miaka ya mbeleni.

Ni wakati wa Watanzania kuona umuhimu wa kujiunga na bima ya afya kama hitaji la lazima ili kuepuka changamoto kwa siku zijazo kutokana na gharama za matibabu kuzidi kuongezeka kila kukicha.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo Taasisi ya JKCI ilianzishwa Septemba 5, 2025 na hadi sana ina uwezo wa kulaza wagongjwa takriban 157 kwa wakati mmoja. Hivyo, kuhudumia, kila wiki, wagojwa 1,800 pamoja na karibu wengine 100 kutoka nchi jirani.

Kwa hali hiyo wataalamu wake wako katika hekaheka za kila wakati kutibu magonjwa ya moyo. Kadhalika, wanawajibika hufanya tafiti mbalimbali kuhusiana na athari kutokana na magonjwa ya moyo lakini pia kufundisha MUHAS.

Mmoja wa wataalamu bingwa wa JKCI, Dk. George Longopa, anayeshughulikia maradhi ya moyo, anasema taasisi imejitokeza kuwa kituo muhimu cha maradhi ya moyo katika Ukanda wa Africa Mashariki na Kati. Mtaalamu anaongeza kuwa taasisi ina vitendea kazi vya kisasa mfano 'cathy-lab, vyumba viwili vya kufanyia upasuaji, na komoja cha kisasa cha wagonjwa mahututi.

Vilevile, taasisi ina watumishi waliohitimu kwa viwango vya juu na wanaojitoa kuwahudumia wagojwa ipasavyo, katika kuyatimiza majukumu yake, JKCI inafanyakazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufikia malengo waliyojiwekwa kitaifa lakini pia yale ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Katika jitihada hizo, Dk. Longopa, anaeleza kuwa JKCI imekuwa ikipokea wagonjwa kutoka nchi jirani mathalani, Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kenya, Malawi, Uganda, Rwanda, Somalia, Sudan, Uganda, Zambia na Zimbabwe".

Licha ya mafanikio makubwa ya JKCI tangu kuanzishwa 2015 na kwa kuzingatia niliyoyaona nilipotafuta huduma mwaka 2016, 2018 na sasa, taasisi inatoa huduma muhimu kwa wenye changamoto za magonjwa ya moyo. Hata hivyo kwa uchunguzi wa haraka, hali ya jumla inaonyesha inafanyakazi katika mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na eneo dogo sana taasisi ilipo kulingana na majukumu yake.

Hospitali ya Mloganzila ina eneo kubwa kadhalika, kwa mtazamo wangu, eneo hilo linaweza kutosheleza mahitaji ya JKCI, hivyo, kuiwezesha kufanya maendeleo makubwa zaidi kimatibabu, kitaaluma na kijamii.

Kwa kulinganisha taasisi hizo mbili, licha ya ukweli kwamba zinashughulikia matibabu ya binadamu, hata hivyo, kwa eneo lililopo Mloganzila, JKCI ingekuwa katika nafasi ya kufanya makubwa zaidi kitabibu na kimaendeleo. Kwa sababu shughuli za JKCI zimepanuka sana kulinganisha na ilivyoanza, kwa mtazamo huo, ni dhahiri kuwa umuhimu wa JKCI kupata sehemu kubwa ili kupanua zaidi kazi zake haikwepeki.

Aidha, nafasi ya kufanyia kazi pamoja na kuweka vifaa katika jengo lililopo Muhimbili, ni finyu, hivyo kutokana na ongezeko la wagonjwa wa maradhi ya moyo JKCI inahitaji kuwezeshwa kuongeza ufanisi kuhudumia wagonjwa ipasavyo.

Lakini pia ili JKCI iweze kuboresha huduma zake na kufanya vizuri zaidi, hivyo serikali iangalie uwezekano wa kuipa nafasi kwenye Hospitali Mloganzila.

Jambo jingine ni JKCI ina msongamano wa wagonjwa hususani kwenye baadhi ya maeneo. Mathalani, chumba kidogo sana cha maabara, vilevile, kuna vyumba vingine pia vidogo vya kufanyia vipimo mbalimbali.

Mfano, kumchunguza mgonjwa kupitia: ECG, ECHO, kupima kiwango cha 'stress', na kufanya 'ambulatory recording'.

Changamoto zinazoikabili JKCI, kwa kiasi kikubwa, zinasababishwa na ufinyu wa sehemu za kutolea huduma kwa wagonjwa. Je, tuache hali hiyo iendelee? Nafikiri ni vema tufanye jitihada za kukabiliana na hali hiyo mara moja. Ni vyema kuangalia uwezekano kwa vituo viwili JKCI na Mloganzila kubadilishana maeneo.

Baada ya uamuzi kufikiwa, JKCI itakuwa na uwezo mkubwa wa kuongeza nguvu katika huduma kwa magonjwa ya moyo. Hayo yatakuwa mafanikio, kwa wakati muafaka, siyo kwa Tanzania tu bali pia Afrika ambayo inatumia hospitali hiyo.

Kupata eneo Mloganzila kunazingatia kuepuka ucheleshaji usio wa lazima, katika kutafuta maeneo mengine yanayofaa.

Kadhalika, uanzishaji wa vituo vipya utatumia muda mrefu na kughubikwa sintofahamu nyingi kutokana na madhaifu na makosa ya kibinadamu kwa kudhamilia au bahati mbaya, wakati maradhi ya moyo na mishipa ya damu yanazidi kuwa changamoto kubwa nchini na barani Afrika.

Majira yanakimbia, kinachowezekana kufanyika sasa kitaweza kuisogeza Tanzania na Afrika mahali pazuri ili kukabiliana na magonjwa ya moyo kwa ufanisi zaidi.



# Wanawake wapewa angalizo la matumizi neno 'haki sawa'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE wameaswa kuwa waangalifu katika matumizi ya neno haki sawa ili lisisababishe migogoro kwenye familia.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na wakili kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Isabela Nchimbi, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani katika Kata ya Mpunguzi jijini hapa.

Nchimbi alisema kumekuwa na mkanganyiko kwa baadhi ya maeneo kutokana na wanawake kujisahau wakati mwingine na kujikuta wakililia haki ambazo kimsingi hawawezi kuzipata na kukwepa majukumu yao ya msingi.

Wakili huyo alishauri elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wanawake ili watafute haki kwa njia nzuri isiyosababisha migogoro kwa familia.

"Baadhi yetu tukirudi majumbani tunaacha majukumu yetu ya msingi kwa kisingizio cha haki, ni kweli kwamba tunaitafuta haki hiyo lakini lazima tuwe makini ni kwa jinsi gani tunastahili," alisema Nchimbi.

Naye Diwani wa Kata ya Mpunguzi, Innocent Nyambuya, alikiri kuwa wanapokea malalamiko mengi kuhusu wanawake kusahau majukumu ya kutaka wafanyiwe na wanaume.

Nyambuya alisema neno haki sawa linatumika kwa faida lakini upande mwingine linakuwa na hasara zake kwa kuwa baadhi wanataka haki hata kwa mambo yasiyokuwa ya haki.

"Hili neno haki sawa au hamsini kwa hamsini kwa baadhi ya maeneo limeanza kutupa shida, mtu anatamani kufanyiwa majukumu ambayo hata Mwenyezi Mungu hakumpa majukumu hayo mwanaume kuyafanya," alisema Nyambuya.

Mkazi wa Mpunguzi, Rehema Wami, alisema haki za wanawake kwa maeneo ya vijijini bado ni tatizo lakini wengi hawajui kwa namna gani wanaweza kuzipata.

Rehema alitolea mfano umiliki wa mali ikiwamo mauzo ya mazao kama zabibu ambazo wanalima wote lakini ukifika wakati wa kuuza au kupokea fedha jina linaloandikwa ni mwanaume na ndiye anakwenda kupokea fedha hizo.

## TUICO yawakumbuka watoto yatima Siku ya Wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) imetoa msaada wa mahitaji muhimu kwa kituo cha watoto yatima cha Dunia Heri.

Akizungumza baada ya kuwasilisha msaada huo, Mkuu wa Idara ya Wanawake, Afya na Usalama na Watu wenye Ulemavu kutoka TUICO, Witness Mwijage alisema wanawake ndio nguzo imara katika familia na jamii, hivyo wanapaswa kuwasaidia watu wenye uhitaji.

Alisema wanawake kutoka TUICO wameugana na wanawake wengine duniani kote katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kutoa msaada kwa watoto yatima.

"Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tumeguswa sisi kama wanawake kuja kusherehekea siku hii na watoto wa kituo hiki cha Dunia Heri, hivyo tumeguswa kutoa matendo ya huduma kwa watoto wanaoishi katika kituo hiki," alisema.

Witness alisema: "Tumeguswa kutoa msaada wa vitu mbalimbali katika kituo hiki. Kwetu sisi haya ni matendo ya huruma ukizingatia kipindi hiki ni cha Kwaresma kwa Wakristo na Ramadhani inakuja".

Akitaja baadhi ya vitu ambavyo walitoa katika kituo hicho ni pamoja na mchele, unga, sukari, maji, sabuni, chumvi na vitu vingine mbalimbali.

Aidha, aliushukuru uongozi wa TUICO pamoja na wadau wengine ambao wameweza kuwaunga mkono na hatimaye kufanikisha wanawake hao kuwafikia watoto wa kituo hicho.

Pia alitoa wito kwa wanawake wengine kuinga mfano wa wanawake hao wa kuwa na utaratibu wa kutoa matendo ya huduma kwa watu mbalimbali wasiojiweza.

Msimamizi wa kituo hicho, Beata Kusel aliushukuru uongozi wa wanawake wa TUICO kwa kuwapatia vitu mbalimbali jambo ambalo limewapa faraja.

Alisema kituo hicho kina watoto 37, huku watoto 15 wakiwa ni wanafunzi.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata (kulia), akimtwisha ndoo ya maji Zainabu Juma baada ya kutembelea mradi wa maji wa Kijiji cha Semfunga, Halmashauri ya Wilaya ya Singida juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Dk. Mpango: Matumizi ya gesi yatasaidia kuacha kuni, mkaa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameipongeza kampuni ya Taifa Gas kwa kutoa mitungi ya gesi 10,000, akisema hatua hiyo itasaidia kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Alitoa pongezi hizo wakati wa kongamano la wanawake la kuhimiza matumizi ya nishati safi lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini hapa.

Dk. Mpango alisema wadau mbalimbali ikiwamo kampuni hiyo imeendelea kusaidia ajenda ya nishati safi na kwamba kutolewa kwa mitungi hiyo kutawatua wanawake kuni kichwani.

Meneja Mkuu wa Taifa Gas, Devis Deogratius, baada ya kukabidhi mitungi hiyo aliipongeza serikali kwa juhudi zake za kupambania Watanzania ili wawe miongoni mwa nchi ambazo zinatamba duniani katika kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia alisema kuwa mikakati ya kampuni yao ni kuhakikisha upatikanaji wa gesi unakuwa mwepesi na kumfikia kila mtu nyumbani.

# Wajumbe wahoji 'kupotea' mtambo wa kuchimba visima

**Na Elisante John,** SINGIDA

WAJUMBE wa kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa wa Singida (RCC), wamehoji kukosekana kwa mtambo wa kuchimbia visima vya maji virefu uliotolewa na serikali mkoani hapa, ili kusaidia kutatua tatizo la maji kwa wananchi.

Katika kikao hicho kilichoketi juzi, mmoja wa wajumbe ambaye ni Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alisema Wakala wa Majisafi Mijini na Vijijini (RUWASA) mkoa unazembea kutatua kero ya maji, hasa maeneo ya vijijini licha ya serikali kuupatia mkoa mtambo wa kuchimbia visima virefu.

"Mwenyekiti naomba kujua ule mtambo wetu wa kuchimbia visima virefu, tulioletewa na Rais, Je, ni kwa ajili ya mkoa wetu wa Singida? au ni la mikoa mingine zaidi, naomba kufahamishwa hili, kwa sababu tunapohitaji tuchimbiwe visima, tunaelezwa gari lipo mikoa jirani, linaendelea kufanya kazi huko," alihoji Mtaturu.

Alisema kukosekana kwa mtambo huo mkoani Singida, kunadhoofisha matarajio ya wananchi kukabiliana na tatizo la maji, katika maeneo ya vijijini, hususani kwenye jimbo lake.

Aidha, alihoji kusuasua kwa mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile, katika Wilaya ya Manyoni, ambao ukikamilika mapema utamaliza tatizo la maji, kwa wananchi wanaoishi kwenye Bonde la Kintinku, wilayani Manyoni.

Aliitaja miradi mingine inayohitaji nguvu kubwa ya RUWASA hadi kukamilika na kuanza kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Ikungi ni mradi wa Minyinga, Sakaa na Mkunguwakihendo, inayosuasua kwa muda mrefu, hivyo kufifisha matumaini ya wananchi kupata huduma ya maji safi na salama.

Akijibu hoja hizo, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Singida, Lucas Said alisema gari la mtambo wa kuchimbia visima virefu kiuhalisia ni la Mkoa wa Singida.

Alisema lakini ilibidi likahudumie mkoani Manyara kwa agizo la Serikali, kufuatia janga la maporomoko ya udongo Katesh, wilayani Hanang, lakini limesharejea na linaendelea kutumika katika Wilaya ya Mkalama.

Hata hivyo aliomba ushirikiano kutoka halmashauri zote za wilaya ili ziwe zinatenga fedha angalau kidogo kutoka mapato ya ndani, badala ya bajeti yote kuachiwa RUWASA.

"Kabla ya Rais kutuletea mtambo huu, gharama ya kuchimba kisima kimoja ilikuwa ni kati ya Sh. milioni 33 mpaka Sh. milioni 40, lakini sasa hivi ni Sh. milioni 20 hadi Sh. milioni 23...naziomba halmashauri zetu za wilaya, tushirikiane nazo ili kumaliza kero hii ya maji, kwa watu wetu," alisema.

Kuhusu kuchelewa kwa mradi wa Kintinkuusile uliopo wilayani Manyoni, alisema hadi sasa umefikia asilimia 90, lakini unakwama kukamilika kutokana na deni la Sh. bilioni nne ambazo mkandarasi anaidai Serikali.

Alisema hivi sasa huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama maeneo ya vijijini, umefikia asilimia 67.7.



# Gereza la Kilimo Songwe kinara uzalishaji chakula

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

GEREZA la Kilimo la Songwe lililoko mkoani hapa limetajwa kuwa ndilo linaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini, hali inayolifanya kulisha magereza mengine yaliyoko katika mikoa nane.

Mkuu wa gereza hilo, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Stockwell Mlyuka aliyasema hayo juzi mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya walimu wa shule za msingi na sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya waliokwenda kwa lengo la kutoa misaada kwa wafungwa.

Alisema gereza hilo ni miongoni mwa magereza 24 nchini ya kimkakati kwa ajili ya uzalishaji na kwamba wao wanazalisha zaidi mahindi kutokana na hali ya hewa na eneo lililopo.

Alisema wamekuwa wakiongeza eneo la uzalishaji kila mwaka kulingana na idadi ya wafungwa ambao wanatumika kama nguvu kazi pamoja na uboreshaji wa teknolojia.

Alisema kwa msimu uliopita walilima ekari 900, lakini msimu huu wameongeza eneo la uzalishaji na kufikia ekari 960 ambazo zote wamelima mahindi.

"Sasa chakula ambacho tumekuwa tukizalisha tumekuwa tukilisha magereza yote ya mikoa ya Iringa, Morogoro, Pwani, Shinyanga, Dar es Salaam, Dodoma Mbeya yenyewe na magereza yote ya Mkoa wa Songwe isipokuwa gereza moja pekee la Ngwala," alisema Mlyuka.

Alisema gereza hilo limekuwa likipokea wafungwa kutoka katika mikoa mbalimbali ya nchi ikiwamo mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kusini hali ambayo inasababisha wengi kushindwa kutembelewa na ndugu zao na kupelekewa mahitaji.

Aliwashukuru walimu hao kwa msaada wa vitu walivyopeleka akieleza kuwa vitawasaidia wafungwa hao katika kipindi ambacho watakuwapo ndani ya gereza hilo wakitumikia vifungo.

Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Wilaya ya Mbeya Vijijini, Mwalimu Judith Mangi alisema misaada waliyotoa ilitokana na michango ya walimu wanawake ambao walikubaliana kwenda kuwafariji wafungwa ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Aliitaja misaada waliyotoa kuwa ni magodoro, mafuta ya kupikia na ya kupakaa, sabuni, miswaki na dawa za miswaki kwa ajili ya wafungwa hao.

Aliwaomba wadau mbalimbali kuendelea kuungana nao kwa ajili ya kuwatembelea wafungwa hao na kuwapatia vitu mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wawapo gerezani humo.

"Nawapongeza sana walimu wenzangu kwa kujitoa kwao, tunawaomba na wadau wengine watushike mkono katika kulisaidia kundi hili kwa sababu eneo hili ni kwa ajili ya kurekebisha tabia za watu waliokosea kwenye jamii," alisema Mwalimu Judithi.

Mwenyekiti wa Kitengo cha Wanawake CWT, Mwalimu Agatha Sumbi, alisema wengi wamekuwa wakiwatembelea wanawake pekee walioko kwenye magereza lakini wao waliamua kwenda katika gereza la wanaume kutokana na kwamba wengi wao ni watoto wao na wengine ni waume zao.




Walimu wakike wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiwa pamoja na maofisa wa Jeshi la Magereza walipotembelea na kutoa misaada ya vitu mbalimbali kwa wafungwa wa Gereza la Kilimo la Songwe lililoko mkoani Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TTB yahimiza elimu ya uzalishaji tumbaku yenye viwango

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BODI ya vyama vya ushirika vya wakulima wa tumbaku nchini, imetakiwa kutoa elimu kwa wakulima kuhusu namna bora ya kuzalisha tumbaku yenye ubora na inavyokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje, ili kukuza uchumi wao na taifa.

Mkurugenzi wa tumbaku kutoka Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Nicholaus Mauya alitoa ushauri huo jana alipoongoza timu ya tathmini ya zao hilo kwa vyama vya ushirika vya Igangwe na Mtanila kwenya mkoa wa kitumbaku Chunya.

"Ni muhimu sana kuhakikisha tunaenda sambamba na mahitaji ya soko, hivyo sisi kama viongozi tuendelee kutoa elimu kwa wakulima wetu ili wazingatie ubora na viwango vinavyohitajika vya uzalishaji wa tumbaku ili masoko yatakapoanza wakulima wetu wauze kwa bei nzuri," alisema Mauya.

Meneja wa tumbaku Kanda ya Iringa, Mohamed Kifuniko, aliwataka wakulima wa zao hilo kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalamu ili kuongeza tija ya uzalishaji.

Meneja uendeshaji kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha Tumbaku Chunya (CHUTCU), Juma Shinshi, aliyetaka kampuni ya ununuzi wa tumbaku kuelimisha wakulima, kupanga madaraja ya tumbaku kwa vitendo na sio kwa nadharia.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Mtanila, Ayubu Hussein, aliahidi kuwasimamia wakulima wao katika hatua zote ili kuhakikisha hawaathiri ubora unaohitajika sokoni na hatimaye wakulima wapate bei stahiki ambayo itawapa faida.

# 'Kaya zinazoongozwa na wanawake zinaongoza kwa umaskini'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI kubwa ya kaya zinazoongozwa na wanawake kama wakuu wa kaya zimetajwa kuwa maskini zaidi kutokana na wengi kutokuwa na utamaduni wa kuwekeza vizuri kwenye shughuli za uzalishaji na badala yake kuwa tegemezi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jokate Mwegelo, aliyasema hayo juzi aliposhiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya (CUoM) kilichopo jijini Mbeya.

Alisema taarifa hizo ni kwa mujibu wa taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na kwamba takwimu hizo pia zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya wanawake hawashiriki kwenye siasa, hali ambayo inasababisha kuwa na idadi ndogo kwenye vyombo vya maamuzi.

Alisema kitendo cha wanawake kutoshiriki kwenye siasa kinasababisha mambo mengi yanayowahusu wao yaamuriwe na wanaume na hivyo kuwasababishia maendeleo duni.

Jokate aliwataka wanafunzi wa kike walioko kwenye vyuo mbalimbali kuwa chanzo cha mabadiliko kwenye jamii kwa kutumia elimu wanayoipata.

"Nawaomba wanawake wenzangu tujitafakari nafasi yetu kwenye jamii, serikali inawekeza kwa kiasi kikubwa kwetu hivyo na sisi tunatakiwa tuonyeshe matokeo," alisema Jokate.

Makamu Mkuu wa Chuo cha CUCoM, Prof. Romward Haule, alisema asili ya Siku ya Wanawake Duniani ni harakati za wanawake kudai haki zilizokuwa zinafanyika barani Ulaya.

Alisema wakati huo kulikuwa na tofauti ya mishahara kati ya wanawake na wanaume kwa sifa ambazo zinafanana na kwamba hali hiyo ilisababisha kuanzishwa siku hiyo.

"Siku ya leo ni mwafaka sana maana kwa wanafunzi na wafanyakazi wa chuo chetu hasa wanawake, tunaamini kwamba ujio wako Katibu Mkuu wa UWT utakuwa chachu kwa vijana wetu," alisema Prof. Haule.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliwataka wanawake katika mkoa huo kuungana na kuhakikisha wanashiriki vyema kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema wanawake wanatakiwa kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.



# Benki yamwaga madawati, viti, meza kwa chuo, skuli Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

BENKI ya NMB imetoa msaada wa madawati 307 kwa skuli tatu za msingi pamoja na viti 100 na meza 100 kwa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume (KIST), vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 33.

Msaada huo umetolewa kwa lengo la kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuboresha sekta ya elimu.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa mwishoni mwa wiki iliyopita, NMB ikimkabidhi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa madawati 100 kwa ajili ya Skuli ya Uzini, madawati 150 ya Skuli ya Kidimni na mengine 57 ya Skuli ya Makadara pamoja na viti 100 na meza 100 za KIST.

Meneja wa Biashara wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Said Shaame, ndiye aliyekabidhi misaada hiyo kwa Waziri Lela, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla zote kwenye Skuli za Kidimni na Makadara, kisha naye kukabidhi kwa walimu wakuu wa skuli hizo na Mkuu wa KIST.

Makabidhiano yaliyokwenda sambamba na ufunguzi wa madarasa, ofisi ya walimu, fremu za biashara na ukumbi wa mitihani wa Kidimni, zilizojengwa kwa fedha za Mfuko wa Jimbo la Uzini.

Madarasa, ofisi, fremu za maduka na ukumbi wa mitihani zimeigharimu Ofisi ya Mbunge wa Uzini, Hamza Khamis Hamza 'Chillo,' Sh. milioni 52.5, huku hafla ya pili ya makabidhiano hayo ikifanyika jioni katika Skuli ya Makadara, walikopewa madawati 57, sambamba na kuwapa zawadi wanafunzi waliofaulu vizuri.

Akizungumza katika hafla hizo, Waziri Lela alishukuru NMB kwa kujali jamii kupitia Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI). Misaada hiyo imeheshimisha serikali yake, kwa kuwa inakwenda kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na kufundishia kwa walimu wa skuli na chuo hicho.

Alibainisha ya kwamba NMB imesaidia kuongeza kiwango cha ufaulu katika shule za jimbo lake na kuitaka kutowachoka kwa kuwa kadri idadi ya Wazanzibar inavyoongezeka, ndivyo changamoto katika sekta za elimu na afya zinavyoongezeka na hivyo serikali kuhitaji nguvu za ziada kutoka kwa wadau.

Naima Shaame kwa upande wake alibainisha kuwa, changamoto za elimu ni kipaumbele kwa NMB, ambayo kupitia asilimia moja ya faida yake kwa mwaka, imekuwa inarejesha kwa jamii kupitia misaada ya madawati, viti, meza, kompyuta, vifaa vya kuezekea, ujenzi na ukarabati wa madarasa na ofisi.

Naima aliwataka Wazanzibar uchangamkia fursa zitokanazo na ujio wa akaunti nafuu na rahisi isiyo na makato ya mwezi iitwayo NMB Pesa, ambayo inafunguliwa kwa Sh. 1,000 tu, huku akiwataka kuwajengea watoto na wanafunzi visiwani humo utamaduni wa kujiwekea akiba tangu wakiwa wadogo.

Naibu Waziri Hamza Chillo aliishukuru NMB kwa jicho la huruma walilotumia kuiona Uzini kama sehemu sahihi ya kukabidhi misaada yao ya kielimu na kuwataka kutowachoka, badala yake wajiandae kuendelea kuwasaidia wakazi wa jimbo lake katika kutatua changamoto za elimu ya watoto wao.

Akitoa neno la shukrani, Dk. Khamis Khalid Said ambaye ni Naibu Mkuu wa Taasisi, Taaluma, Utafiti, Ubunifu na Ushauri Elekezi wa KIST, alishukuru NMB kwa msaada wa viti 100 na meza 100 za wanafunzi, ambazo zitarahisisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia chuoni kwake.




Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, akizungumza wakati wa mkutano wa 21 wa Taasisi za Fedha ulioandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania kujadili uimarishwaji wa sekta za kifedha ili kukabiliana na changamoto za kiuchumi mwishoni mwa wiki jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'SMZ, SJMT zinatambua umuhimu, mchango wa wanawake'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema serikali zote mbili ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) zinatambua umuhimu na mchango wa wanawake.

Amesema hivyo serikali inachukua hatua za kumlinda mwanamke na kumwezesha katika hatua za maendeleo.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar, wakati akimwakilisha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali mwinyi katika Kongamano la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi lililoandaliwa na Chama cha Kuendeleza Biashara kwa Wajasiriamali Tanzania (TWCC).

Alisema serikali imetunga sera, sheria pamoja na kuridhia na kutekeleza mikataba na maazimio ya kikanda na kimataifa kama vile mkataba wa umoja wa mataifa wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake wa mwaka 1970.

Alisema pia serikali imeridhia Adhimio la Beijing pamoja na Mkataba wa Kimataifa na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika.

Hemed alisema SMZ imeongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi, kwamba marekebisho ya Katiba ya mwaka 2010 yaliongeza asilimia ya viti maalum vya wanawake katika Baraza la Wawakilishi kutoka asilimia 30 hadi 40.

Vilevile alisema serikali imetoa mikopo ya Sh. bilioni 29.2 kwa wajasiriamali 27,184, kati yao 16,091 ni wanawake kwa lengo la kuwaendeleza kiuchumi.

Mwenyekiti wa TWCC (Zanzibar), Tatu Tandu alisema wanawake wa Zanzibar wanatambua uchumi unategemea sekta ya utalii, mazao ya bahari, uvuvi, kilimo cha mwani na wanawake wengi wamejiajiri katika sekta hizo.

Mkurugenzi mkaazi wa Trademark Africa, Elibarik Shammy, alisema katika kipindi cha miaka saba taasisi yake imetoa Dola za Marekani milioni tatu kwa ajili ya kuwawezesha wanawake zaidi ya 20,000.

Mwenyekiti wa TWCC Tanzania, Mercy Sila alisema taasisi hiyo, inaunganisha wanawake kuwa na nguvu na sauti na mikakati ya kuwawezesha kujikwamua kiuchumi na kijamii.

# Wavuvi, wananchi wapewa angalizo uhifadhi wa viumbe baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba (MIMCA), Yassir Ali Haji, kutoka Idara ya Uhifadhi wa Bahari amewataka wavuvi na wananchi kufuata sheria zilizowekwa na mamlaka zinazohusika na uhifadhi wa viumbe wa baharini ikiwamo kiumbe cha baharini (pomboo), ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza kwa viumbe hao.

Akitoa elimu jinsi ya kuangalia pomboo wanapokuwa baharini kwa wadau wa sekta ya utalii, wananchi na wavuvi huko Nungwi na Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja jana.

Alisema viumbe hao wako hatarini kutoweka kwenye hifadhi kutokana na kujitokeza kwa wadau wa utalii na wavuvi kutofuata sheria wakati wanapokwenda maeneo hayo kuangalia pomboo.

Alisema viumbe hao wanahitaji utulivu na hawapendi kelele, hivyo ipo haja kwa wadau hao kufuata sheria ili kuepusha pomboo kukimbilia maeneo mengine.

Aidha alisema viumbe hao ni muhimu kuwepo sehemu za kihistoria na hifadhi kutokana na kuwa kivutio kikubwa cha watalii.

"Viumbe hawa wamekuwa na tabia ya woga wanapokuwa baharini na pia hawapendi kusikia kelele wakati wanapokuwa baharini jambo la msingi kwa wadau wanaokwenda kuangalia viumbe kufuata sheria," alisema.

Pia aliwataka wavuvi kuacha kutupa nanga maeneo hayo ya hifadhi kuepuka kuharibu matumbawe na rasilimali nyingine za baharini.

Ofisa Mazingira ya Bahari, Thuwaiba Kassim Haji, kutoka Idara ya Uhifadhi wa Bahari aliwataka wadau kusoma tabia za pomboo ili kuepuka kuwaondoa katika makazi yao jambo ambalo linaleta shida kwa viumbe hao.

Ofisa kutoka Kamisheni ya Utalii, Ame Nassor Juma, alisema Pomboo ni muhimu kuwapo katika maeneo ya historia na hifadhi za bahari kutokana na fursa ya ajira kwa wananchi wa Zanzibar na kuongeza pato la serikali kupitia utalii.

Wakitoa maoni yao wadau wa sekta ya utalii waliitaka Idara ya Uhifadhi wa Bahari kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wadau wa utalii na wavuvi juu ya umuhimu wa kuhifdhi pomboo kwa kuwa ni miongoni mwa kivutio kikubwa cha watalii.

Juma Makame Sheha ambaye anajishughulisha na kuwatembeza watalii baharini alisema wapo wavuvi ambao hukokota nyavu sehemu za hifadhi na kusababisha kunasa kwa pomboo kitu ambacho siyo kizuri kufanyika katika hifadhi ya bahari.

Hivyo, aliitaka serikali kuweka boti maalum za kufuatilia pomboo wanaokimbilia baharini kuimarisha sekta ya utalii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**KERA ABDALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0359-0130** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIGURUNYEMBE SEKONDARI** mwaka **2013.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/30401/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DILLY HASSAN BAKARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 872 AGY** aina ya **SUZUKI ESCUDO.** Chassis namba TD01W209503. Engine namba **G16A386708.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/9162/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILIP DONALD MAGAMBO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 983BEL, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**DSM/PHQ/RB/29094/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 3019 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE**
**SALMA MUHIDIN KIMEA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY DAMARIS JOSEPH SHAURI**

### GENERAL CITATION

**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named.
Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of March 2024
Dated at Korogwe this 19th day of February 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Piga Simu 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.**
**TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Ramaphosa akosoa upinzani Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa amekikosoa chama kikuu cha upinzani nchini humo, Democratic Alliance (DA) kwa madai ya kwamba kimeomba waangalizi wa Marekani na nchi za Ulaya kufuatilia uchaguzi ujao unaotarajiwa kufanyika Mei 29, mwaka huu.

Chama hicho kilitoa ombi hilo katika barua iliyotumwa siku chache zilizopita kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken na baadhi ya mawaziri wa mambo ya nje wa Ulaya.



Rais Ramaphosa, alinukuliwa na shirika la utangazaji la SABC akisema, barua ya DA kwa serikali ya Marekani bila shaka inakaribia kujaribu kuuza nchi yao kwa mamlaka nyingine duniani.

"Na tuna mashirika ya kikanda duniani kama SADC, Umoja wa Afrika (AU) na tuna Umoja wa Mataifa (UN) pia. Wanakuja kufuatilia chaguzi zetu na sasa kwa taasisi isiyo ya serikali kuuza demokrasia yetu," alisema Rais Ramaphosa.

Chama tawala cha African National Congress (ANC) pia kiliikashifu DA kwa barua hiyo, kikishutumu chama cha upinzani kwa kunadi uhuru wa Afrika.

Aidha, inaelezwa kuwa kura za maoni za makampuni ya utafiti zinaonyesha kuwa sehemu ya ANC ya kura inaweza kushuka chini ya asilimia 50 kwa mara ya kwanza tangu ilipoingia madarakani mwaka 1994, ikichochewa na kuenea kwa kutoridhishwa na hali ya uchumi, huduma za umma na rushwa. **BBC**

# Timu yataja ilichobaini mfungwa kubaka kijijini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TIMU ya uchuguzi iliyoundwa na Jeshi la Magereza nchini kwa ajili ya kuchunguza tuhuma za mfungwa aliyedaiwa kubaka mtoto nje ya gereza, imebaini mfungwa huyo ametenda kosa hilo, hivyo atafikishwa mahakamani.

Mfungwa huyo ambaye anatumikia kifungo chake katika Gereza la Kalilankulukulu, mkoani Katavi, alikuwa anamaliza muda wa kifungo chake cha mwaka mmoja na nusu Aprili mwaka huu. Alikutwa na hatia ya kukutwa akifanya shughuli za kibinadamu hifadhini mkoani Katavi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha Maofisa Magereza nchini, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee Ramadhan Nyamka alisema timu hiyo imebaini mfungwa huyo alitenda kosa hilo, hivyo atapandishwa kizimbani kwa mara nyingine.

Mbali na hilo, Kamishna Jenerali huyo alisema askari ambaye alikuwa analinda wafungwa hao, naye atawajibishwa kwa mujibu wa taratibu zao za kinidhamu kutokana na kuwaacha wafungwa hao, hata wanafanya vitendo viovu ambavyo havikubaliki ndani ya jamii.

"Ninapongeza timu hiyo ambayo imefanya uchunguzi haraka na kutoa majibu hayo ambayo yatasaidia kujua kwamba ukiwa gerezani unaweza kuhukumiwa tena kwa mara nyingine," alisema Kamishna Jenerali.

Alisema Jeshi la Magereza linalaani vitendo hivyo, akiwataka askari magereza kuwa makini pale wanapopewa kazi ya kulinda wafungwa, wasiwaache peke yao kwa kuwa bado ni wahalifu.

Alisema adhabu itakayotolewa kwa askari aliyekuwa anamlinda mfungwa huyo, itakuwa fundisho kwa wengine ambao wanaleta uzembe kazini pale wanapokuwa zamu katika magereza mbalimbali nchini.

Kamishna huyo alisema kuwa Ijumaa iliyopita, faili la uchunguzi lilifikishwa Ofisi ya Mashtaka, hivyo wakati wowote mfungwa huyo atapandishwa kizimbani kwa ajili ya kusomewa mashtaka mapya akiwa anatumikia kifungo chake cha awali.

Alisema tukio alilofanya mfungwa huyo ni matokeo ya uzembe uliofanywa na askari huyo aliyekuwa na wafungwa hao wakati wakitekeleza majukumu yao ya gerezani.

Wiki iliyopita, Nipashe iliripoti tukio hilo la mtoto kudai kubakwa na mfungwa wa gereza hilo aliyekuwa nje ya gereza.

Kaimu Kamishna Msaidizi wa Utawala na Rasilimali Watu (DCP), Jeremiah Katungu, alisema kikao hiko ni utaratibu wa kawaida ndani ya jeshi hilo ambacho hufanyika kila mwaka kujadili mambo mbalimbali ya utekelezaji majukumu yaliyopangiwa.

Alisema kikao hicho pia hutumiwa kufanya tathmini ya utekelezaji ikiwamo kuweka mikakati ya kuleta ufanisi katika utekelezaji majukumu kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa mwongozo.



Kikosi maalum cha Ikulu ya Haiti kikiimarisha ulinzi katika mitaa ya mjini Port-au-Prince. **PICHA: MTANDAO**



## Ukraine yapinga ombi la Papa

**KYIV,** Ukraine

UKRAINE imepinga wito wa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, juu ya kujadili kusitisha vita na Russia, huku Rais Volodymyr Zelenskiy akisema Papa alikuwa akifanya upatanishi kwa mbali na waziri wake wa mambo ya nje akisisitiza kuwa Kyiv haitasalimu amri.

Papa Francis alisema juzi kuwa wakati mambo yanaelekea kuwa mabaya kwa pande zote kwenye mzozo huo, pande moja inapaswa kuonyesha ujasiri wa kusalimu amri kwa kuinua bendera nyeupe na kujadiliana.

Mahojiano ya Papa yaliaminika kuwa ni mara ya kwanza kutumia maneno kama kuinua bendera nyeupe au kushindwa kwa kujadili vita vya Ukraine, ingawa aliwahi kutaja umuhimu wa mazungumzo.

Ilielezwa kuwa Rais Zelenskiy hakumtaja moja kwa moja Papa Francis au maoni yake lakini alitaja wanadini wanaosaidia ndani ya Ukraine.

"Wanatuunga mkono kwa maombi, kwa majadiliano yao na kwa vitendo. Hivi ndivyo kanisa lenye watu lilivyo," Zelenskiy alisema katika ujumbe wa kila usiku kupitia video.

Waziri wa Mambo ya Nje, Dmytro Kuleba, akiandika kwenye mtandao wa X alisema kuwa mtu mwenye nguvu katika mzozo wowote husimama upande wa wema badala ya kujaribu kuwaweka wote kwenye kigezo sawa na kuyaita mazungumzo.

"Bendera yetu ni ya njano na bluu, hiyo ndiyo inafanya tunaishi, kufa na kushinda. Hatutainua hata siku moja bendera nyingine yoyote," alisema Kuleba. **VOA**

# ZIMAMOTO SC WAANIKA MALENGO YA MAKOMBE

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Zimamoto SC wamesema shauku yao kubwa, mosi ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu na kama hilo likishindikana angalau basi wabebe Kombe la FA.

Zimamoto imefanikiwa kutinga hatua ya 16-bora ya michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, kwa kuiondoa Shangani FC kwa jumla ya mabao 2-0 katika hatua ya 32-bora mchezo uliochezwa juzi katika Dimba la Mau B, wakati Kundemba FC wakiwaondoa Maafande wa Polisi FC kwa mikwaju ya penalti 7-6 baada ya dakika 90 kutoshana nguvu kwa kufungana bao 1-1 mchezo uliochezwa katika Dimba la Mau B.

**Kwa matokeo hayo, Zimamoto sasa imeungana na timu nyingine tatu ambazo hapo jana zilitoka na ushindi katika mashindano hayo, kutinga 16-bora.**

Timu hizo ni Uhamiaji FC ambao waliopaswa kucheza na Ujamaa na timu hiyo haikutokea uwanjani wakati Raskane FC nao wakitoka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Black Mamba katika Uwanja wa Cairo huku Paje Star FC nayo ikitinga hatua hiyo kwa kuiondoa Blak Lione FC kwa mikwaju ya penati 4-3 baada ya dakika 90 kutopatikana mbabe.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto SC, Mohmed Hilali, alisema mipango yao ni kuhakikisha wanatwaa kombe mojawapo kati ya hayo mawili kwa msimu huu.

Alisema wataendelea kupambana katika michezo ya Ligi Kuu, lakini pia kuelekeza nguvu na mipango yao katika Kombe la FA ili mwisho wa msimu watimize lengo lao la kutwaa kombe moja wapo.

Hilali alisema ingawa michuano yoyote ya mtoano huwa migumu, lakini wamejiandaa katika kuhakikisha wanafanikiwa kutimiza lengo lao kwa kukabiliana na timu yoyoye watakayocheza nayo katika hatua hiyo ya 16-bora.

"Tunataka na tunatamani kuhakikisha tunatimiza lengo letu kuona hadi mwisho wa msimu tunachukua kombe mojawapo, lengo letu ni Ligi Kuu, lakini ikitokea tukibeba na hili basi bado tumefanikiwa," alisema.

Aidha, alisema kwa muda mrefu hawakuweza kutwaa makombe, hivyo msimu huu ni wao kuhakikisha wanatimiza malengo yao. Timu 16 ambazo zimetinga hatua hiyo ya 16-bora kutoka timu za Ligi Kuu ni Zimamoto SC, KVZ FC, Uhamiaji FC, Kundemba FC, Mlandege FC, Mafunzo SC, JKU SC na KMKM SC.

Kutoka Ligi Daraja la Kwanza ni Kilimani FC, Raskazone FC, Taifa Jang'ombe FC, Black Sailor FC, Inter Zanzibar FC , Paje Star FC, New King FC, na timu moja kutoka Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Nyangobo FC.

## *Waziri Junior mbio moja na Aziz Ki kumsaka Fei Toto*

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa KMC FC, Waziri Junior, amekuja kwa kasi ya kutisha katika mbio za kuwania Kiatu cha Ufungaji Bora Ligi Kuu Bara wakati huu akimfikia kiungo wa mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, mwenye mabao 11, moja nyuma ya kinara Feisal Salum 'Fei Toto' anayeichezea Azam FC.

Waziri juzi alifunga mabao matatu 'hat-trick' katika mechi dhidi ya Tabora United iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na timu yake kushinda 4-2. Alifunga dakika ya 49, 60 na 67 alikamilisha hat-trick yake na kufikisha mabao 11 hadi sasa msimu huu sawa na Aziz Ki.

Akizungumza na Nipashe jana, Waziri alisema lengo lake kubwa ni kusaidia timu yake kupata matokeo mazuri na kwamba suala la ufungaji bora hilo ni la ziada kwake na endapo likitokea litakuwa jambo la kheri.

"Nafurahi kushinda mechi ya leo (juzi), dhidi ya Tabora United, haikuwa mechi rahisi, suala la kufunga ni wajibu wangu kama mshambuliaji, nitahakikisha naisaidia timu kupata matokeo mazuri. Ufungaji bora kama hilo litatokea ni jambo zuri, lakini kwa sasa naangalia zaidi timu yangu kutafuta matokeo. Kabla ya mechi hii tulipanga lazima kujitoa na kuifunga Tabora United na tumefanikiwa tunaenda mapumziko tukiwa hatuna presha," alisema.

Aliongeza kuwa hayuko katika ushindani na mtu yeyote na wanaenda katika mapumziko ya Kalenda ya Fifa wakiwa vizuri. Waziri aliwahi kuicheza Yanga na aliitua hapo akitokea Mbao FC, lakini alikwama kuwa kwenye ubora kutokana na kutopewa nafasi mara kwa mara na hata alipopewa hakuonyesha ubora wake wa kucheka na nyavu kama ilivyo sasa.



Mashabiki wa timu ya mpira wa miguu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), wakiwa na kombe walilotwaa baada ya kushinda kwa penalti 4-3 dhidi ya Polisi Jamii Temeke. Hatua hiyo ya mikwaju ya penalti ilifikiwa baada ya kutoka sare ndani ya dakika 90. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Julio atajwa kocha mpya Singida

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa zamani wa Klabu za Simba, Coastal Union, Mwadui FC na Namungo FC, Jamhuri Kikwelo 'Julio' ametajwa kuwa ndiye atakiongoza kikosi cha Singida Fountain Gate, kuchukua nafasi ya raia wa Afrika Kusini, Thabo Senong, aliyetimuliwa hivi karibuni na benchi lake lote la ufundi.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema Julio huenda akatangazwa rasmi baada ya kumalizika kwa mchezo wa leo kati ya timu hiyo na Simba, ambao utaendelea kusimamiwa na Kaimu Kocha Mkuu, Ngawina Ngawina.

Chanzo kinasema Julio amekuwa chaguo la timu hiyo baada ya kushindwa kumnasa Juma Mgunda ambaye alikuwa ni chaguo la kwanza la viongozi wa timu hiyo.

"Ni kweli tulimtaka Mgunda, hakupatikana, lakini tupo kwenye mazungumzo na Julio, kama tutakamilisha mapema makubaliano tutamtangaza baada ya mechi dhidi ya Simba," kilisema chanzo chetu.

Hivi karibuni timu hiyo ilitimua benchi lote la ufundi kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hussein Massanza, ni kutokana na matokeo yasiyoridhisha kwenye Ligi Kuu.

Timu hiyo imecheza mechi nane bila kupata ushindi, ambapo mara ya mwisho kushinda ilikuwa Novemba 27, mwaka jana, ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1 nyumbani, na hadi leo hii haijaonja ladha ya ushindi ikicheza mechi nane, ikipoteza tano na sare tatu.

Desemba Mosi, mwaka jana, ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, na sare nyingine na mechi inayofuata ikatoka suluhu dhidi ya KMC, kabla ya kwenda kukutana na kipigo cha bao 1-0, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, dhidi ya Geita Gold.

Ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, kabla ya kupata kipigo kingine cha mabao 3-1 dhidi ya Prisons, na kwenda kutoa sare ya bao 1-1, dhidi ya Tabora United.

Baada ya hapo ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Azam kabla ya kubamizwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.



## ZISIKUPITE

### KANE AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United itafanya kila iwezalo kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na England, Harry Kane, 30, iwapo atapatikana msimu huu wa majira ya joto. ***(Give Me Sport)***

### SON MKATABA MPYA

KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo na nahodha Son Heung-min, 31, kuhusu mkataba mpya na wana imani makubaliano na mshambuliaji huyo yatakamilika msimu huu. ***(Football Insider)***

### LIVERPOOL NA MAKOCHA

LIVERPOOL imewachagua Kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi, Kocha wa Ujerumani, Julian Nagelsmann na Ruben Amorim wa Sporting Lisbon kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp. ***(Football Insider)***

### KIMMICH BADO HAKIELEWEKI

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich, 29, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Manchester City na Liverpool, bado hajafanya mazungumzo ya mkataba mpya na Bayern Munich ikiwa imesalia chini ya miezi 18 katika mkataba wa sasa wa mchezaji huyo. ***(90 min)***

### NEVES KUTUA MAN UNITED

MMILIKI mpya wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, anatazamiwa kuidhinisha dau la zaidi ya pauni milioni 100 kwa kiungo wa kati wa Benfica, Mreno Joao Neves, 19. ***(Mirror, via Mail)***

### ARSENAL KUMUUZA TIERNEY

ARSENAL iko tayari kumuuza beki wao, Kieran Tierney, 26, msimu huu wa majira ya joto, lakini 'Washikabunduki' hao wanataka pauni milioni 20 kwa mlinzi huyo wa Scotland. ***(Give Me Sport)***

### GALLAGHER BADO CHELSEA

CHELSEA bado haijafanya maamuzi kuhusu mustakabali wa kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 24, licha ya Tottenham Hotspur kumtaka. ***(Caught offside)***

### MAINOO KUONGEZEWA

MANCHESTER United imenuia kuongeza mshahara wa kiungo wa kati wa England, Kobbie Mainoo, 18, mara tatu chini ya mwaka mmoja baada ya kusaini mkataba mpya, ili kumbakisha klabuni hapo hadi mwaka 2030. ***(Sun)***

### KIWIOR ATAKIWA MILAN

AC Milan bado inafanya mazungumzo na Arsenal kuhusu uhamisho wa beki wa Poland, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 24. ***(Fichajes, via Team Talk)***

### CHELSEA KUUZA 15

CHELSEA huenda ikawauza wachezaji 15 katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Football.London)***

### NETO AMULIKWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imejadili uwezekano wa kumsajili Pedro Neto, 23, kutoka Wolves msimu huu, kwa dau la takriban pauni milioni 60 inayodhaniwa kuwa inatosha kumsajili winga huyo wa Ureno ingawa Liverpool pia wanamtaka. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AKERWA REFA EPL KUINYIMA LIVER PENALTI

**LIVERPOOL,** England

**Watu wote walio na iPads karibu nami walikuwa, 'Wow, wazi', labda wanaweza...**

JURGEN Klopp amesema Liverpool walinyimwa penalti ya wazi na akahoji alichokuwa akifanya Ofisa wa VAR, Stuart Attwell, baada ya Alexis Mac Allister kupigwa teke la kifua dakika ya 99 na Jeremy Doku wa Manchester City katika sare ya bao 1-1 Jumapili kwenye Uwanja wa Anfield.

**Mkwaju wa penalti wa Mac Allister kipindi cha pili, baada ya kipa wa City, Ederson kumchezea vibaya Darwin Nunez, ulipa pointi moja Liverpool baada ya John Stones kuwapa mabingwa hao uongozi wa kipindi cha kwanza.**

Lakini Liverpool wangeweza kupewa nafasi ya kushinda mchezo dakika za lala salama kama mwamuzi Michael Oliver angekwenda kukagua VAR kwa faulo ya Doku.

Tukio hilo lilitathminiwa na Attwell na msaidizi wa VAR, Nick Hopton, lakini Oliver hakwenda kuangalia tukio hilo ili kufanya uamuzi wa mwisho.

"Kwa nini mtu aliye kwenye chumba cha VAR afikiri kwamba hilo haliko wazi?" Alihoji Klopp. "Alikuwa na chakula gani cha mchana?"

"Ilikuwa penalti kwa asilimia 100. Watapata maelezo. Ilikuwa ni faulo kwa asilimia 100 katika maeneo yote ya uwanja na pengine kadi ya njano.

"Mtu atanieleza namna gani haikupaswa kuwa penalti, au Howard (Webb, mkuu wa waamuzi) atanipigia simu kesho na kuniambia samahani. Haya ni matokeo mawili yanayowezekana na mambo yote mawili hayatabadilisha matokeo.

"Watu wote walio na iPads karibu nami walikuwa, 'Wow, wazi.' Labda wanaweza kujificha nyuma ya kifungu kisicho wazi na dhahiri.

"Bila shaka ni penalti, lakini hatukuipata na hiyo ni sawa. Jambo muhimu zaidi kwangu ni kwamba tunaweza kucheza soka. Nimeona maonesho mengi ya kustaajabisha."

Sare hiyo inaifanya Liverpool kuwa mbele ya Man City kwa pointi moja, lakini pointi moja nyuma ya vinara Arsenal katika mbio za kuwania ubingwa. City watacheza na Arsenal kwenye Uwanja wa Etihad Machi 31, mwaka huu.

Kutokana na kukosekana kwa wachezaji kadhaa muhimu kwa sababu ya majeraha, Klopp alijawa na sifa tele kwa timu yake kupata sare kwenye uwanja wa Anfield.



# GUARDIOLA AELEZA HASIRA YA DE BRUYNE KUTOLEWA

**LIVERPOOL,** England

PEP Guardiola amesisitiza kwamba hasira ya Kevin De Bruyne kutolewa nje wakati Manchester City ilipotoka sare ya 1-1 na Liverpool ilikuwa ni jambo "zuri".

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji alianza mchezo katikati ya safu kiungo pamoja na Rodri na Bernardo Silva, lakini baada ya dakika 30 alitengeneza bao la John Stones. Lakini Kocha wa Man City, Guardiola, aliamua kumtoa De Bruyne na kumuingiza Mateo Kovacic katika dakika ya 69 ya mchezo huo.

De Bruyne alioneshwa kukasirishwa na uamuzi huo, akitoleana maneno na maofisa wa klabu hiyo alipokuwa akitoka nje ya uwanja. Akizungumza na Sky Sports baada ya tukio hilo, Guardiola alisema maneno ya kiungo huyo yalikuwa mazuri, akisema: "Hiyo ni nzuri."

"Atakuwa na nafasi katika mchezo ujao kuthibitisha jinsi nilivyokosea, hivyo wakati ujao atakuwa nayo. Ni sawa.

"Tulihitaji mchezaji ambaye alikuwa na mpira na angeumiliki. Si juu ya kushinikiza, si juu ya mchezo huu na ndio maana Mateo Kovacic ni mzuri pamoja na Bernardo Silva ambao wanamchezesha Phil.

"Katika nafasi zingine, anaweza kushika mpira na kupiga pasi ya ziada, kufika kwenye eneo la hatari.

"Phil (Foden) alifika mara mbili au tatu kwenye lango la wapinzani na katika nafasi ya tatu ya mwisho, kwa sababu najua katika nafasi Phil zinaweza kuwa mabao."

# Kimmich bado hajajua mustakabali wake Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

JOSHUA Kimmich amesisitiza kuwa ametulia kuhusu mustakabali wake na Bayern Munich, lakini bado hajafanya mazungumzo kuhusu hali ya mkataba wake.

Kimmich ameingia miezi 18 ya mwisho ya mkataba wake na amekuwa akihusishwa na kuhamia Ligi Kuu England, ambapo miamba kama Manchester United, Manchester City na Liverpool zote zimetajwa kuwa na nia ya kumsajili.

"Kwa ujumla, hali yangu iko wazi," alisema Kimmich baada ya ushindi wa Bayern wa 8-1 dhidi ya Mainz.

"Bado nina zaidi ya mwaka mmoja kwenye mkataba wangu. Hakuna mtu ambaye amezungumza nami. Ndiyo maana nimepumzika sana.

"Hebu tuone nini kitatokea. Kwangu, jambo muhimu zaidi ni kwamba ninafanya vizuri, kwamba nifikie uchezaji wangu wa juu, na siwezi kushawishi wengine."

Mustakabali wa Kimmich pia uliwekwa kwa Mkurugenzi wa Bayern, Max Eberl, ambaye alikiri klabu hiyo inahitaji kujua ni nani atakuwa kocha wao ajaye kabla ya kufanya uamuzi kuhusu hali ya mkataba wa Kimmich.

"Ni mchezaji muhimu sana na anayestahili Bayern Munich," alisema Eberl akiiambia Sky Sports.

"Pia itategemea na kocha mpya na jinsi atakavyomwona Josh. Kwa sasa anahitajika kwenye safu ya ulinzi, ambapo anafanya vizuri sana na ni msaada mkubwa kwetu. Lakini pia Josh ni mchezaji wa kiungo.

"Lakini nadhani kocha mpya anaweza kuwa na maoni tofauti na kumwona mchezaji kwa njia tofauti. Kimsingi, unapaswa kusubiri na kuona."



# Barca yakataa ofa ya Mil. 200 kwa Yamal



**BARCELONA,** Hispania

PARIS Saint-Germain wametoa ofa ya euro milioni 200 kwa winga Lamine Yamal, lakini imekataliwa na Barcelona, kwa mujibu wa ripoti.

PSG wanajiandaa kuondoka kwa Kylian Mbappe, ambaye ataondoka msimu huu wa majira ya joto baada ya kumalizika kwa mkataba wake na anatarajiwa kujiunga na Real Madrid.

Licha ya kumpoteza Mfaransa huyo kwa uhamisho wa bure, makubaliano ya kisheria kati ya klabu na mchezaji huyo yatamfanya Mbappe kulipa hadi euro milioni 80 atakapoondoka.

Kuondoka kwa Mbappe pia kutaifanya PSG kuokoa karibu euro milioni 200 kila mwaka, na kuwaacha na fedha nyingi kusajili mbadala wa jina kubwa.

Na kwa mujibu wa gazeti la Marca, PSG wameweka macho yao kwa Yamal.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 16, ameibuka kama mchezaji muhimu wa Barcelona msimu huu, akifunga bao lake la sita msimu huu, Ijumaa wakati Barca wakiibamiza Mallorca kwenye LaLiga, ambapo Yamal alijikuta akifananishwa na Lionel Messi.

Aina hiyo ya vipaji, ndivyo PSG wanatafuta na inasemekana waliweka wazi kwa Barcelona kwamba watakuwa tayari kulipa euro milioni 200 ili kumnasa Yamal kwenda Ufaransa msimu huu wa majira ya joto.

Wakala wa Yamal, Jorge Mendes, alikutana na rais wa Barcelona, Joan Laporta, mapema wiki hii kujadili mada kadhaa na pendekezo hili kutoka kwa PSG kwenye ajenda.

Barcelona, ambao tayari walikuwa na ufahamu wa kutoka kwa PSG, waliweka wazi kwamba hawana mpango wa kumuuza Yamal msimu huu wa majira ya joto.

Wakiwa na wasiwasi wa aina ile ile ya uwezo wa kifedha ambayo PSG ilianzisha kifungu cha Neymar cha euro milioni 222 mnamo 2017, Barcelona iliingiza kifungu cha kumnunua cha euro bilioni moja katika mkataba wa miaka mitatu aliosaini Lamal mwaka jana.

Kuhusu PSG kutafuta mbadala wa Mbappe, 90min inaelewa Marcus Rashford wa Manchester United na Victor Osimhen wa Napoli pia ni wachezaji wanaozingatiwa.

# Gamondi ambwaga Benchikha

Na Adam Fungamwango

GOLIKIPA wa Timu ya Coastal Union, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ley Matampi, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Februari, huku Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi akiibuka kuwa kocha bora.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), washindi hao wamechaguliwa na Kamati ya Tuzo, ambayo pia imemchagua Meneja wa Uwanja wa Azam Complex, Amir Juma, kuwa meneja bora wa mwezi huo.

Kwa mujibu wa kamati hiyo, Matampi amewashinda Mudathir Yahaya wa Yanga na Samson Mbangula wa Prisons, huku Muargentina Gamondi akiwabwaga Abdelhak Benchikha wa Simba na Kocha Mkuu wa Prisons, Ahmad Ally.

Kipa huyo ametwaa tuzo la uchezaji bora wa mwezi baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwa kucheza dakika 270, sawa na michezo mitatu bila kuruhusu bao ndani ya mwezi huo, wakitoka suluhu dhidi ya KMC ugenini, ikishinda nyumbani bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji na kupata ushindi kama huo dhidi ya Mtibwa Sugar.

Takwimu zinaonyesha pia kuwa kipa huyo ndiye anayeongoza kwa kukaa langoni mechi nyingi bila kuruhusu bao, akifanya hivyo mara tisa, akifuatiwa na kipa wa Tabora United raia wa Nigeria, John Noble mwenye 'clean sheets' saba.

Kwa upande wa Gamondi, taarifa imeeleza kuwa aliiongoza Yanga katika michezo mitano, ikishinda minne na kutoka sare mmoja, ikipanda kutoka nafasi ya pili hadi ya kwanza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# AUCHO AIPA PIGO YANGA ROBO FAINALI MECHI CAF

Na Saada Akida

WAKATI droo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikipangwa leo na kisha mechi za hatua hiyo zikitarajiwa kupigwa kati ya Machi 29-31, mwaka huu, kiungo mkabaji na tegemeo kubwa katika kikosi cha kwanza cha Yanga, Khalid Aucho, ataikosa mechi hiyo, imefahamika.

Yanga na Simba zote zimefuzu hatua ya robo fainali, na katika droo ya leo itakayofanyika nchini Misri saa tisa alasiri, vijana wa Miguel Gamondi wanaweza kuangukia kwa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ama Petro de Luanda ya Angola.

Kwa upande wa kikosi cha Abdelhak Benchikha (Simba), wenyewe hatua hiyo wanaweza kupangwa na Al Ahly ya Misri, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ama Petro de Luanda ya Angola.

**Kuelekea mechi za hatua hiyo, Aucho hatakuwa sehemu ya kikosi, kutokana na kutakiwa kuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki tatu kuanzia juzi, akiuguza jeraha lake goti la kushoto baada ya kufanyiwa upasuaji mdogo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Aucho alisema hatakuwa sehemu ya kikosi cha Yanga kwa muda wa wiki tatu kwa ajili ya kuuguza jeraha lake na baada ya hapo ataanza kufuata maelekezo ya madaktari juu ya programu ya mazoezi.

Alisema anawashukuru wote waliompa pole na kumwombea apone haraka na kuweza kurejea katika ubora wake na kuungana na wachezaji wenzake kwa ajili ya mapambano yaliyopo mbele yao.

"Nashukuru wananchi kwa dua zao kipindi chote cha upasuaji mdogo wa goti, nimeruhusiwa nitakuwa nje ya uwanja kwa muda kwa ajili ya kuuguza jeraha, ninaimani kwa kipindi nilichopewa nitakuwa fiti na kurejea uwanjani kuendelea na mapambano," alisema kiungo huyo.

Aliongeza kuwa kipindi chote atakachokuwa nje atakuwa na programu maalum kwa ajili ya kujiweka fiti kabla ya kurejea uwanjani katika mazoezi mepesi na ya ushindani.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wataendelea kumkosa kiungo huyo katika michezo miwili iliyosalia ya Ligi Kuu kwa sababu ya kuuguza jeraha lake.

"Ni kweli tutamkosa Aucho kwa muda wa wiki tatu nje ya uwanja kwa sababu ya jeraha lake baada ya kufanyiwa upasuaji mdogo wa goti, atakuwa chini ya uangalizi wa daktari kwa kipindi chote atakachokuwa nje na kuanza kwake mazoezi mepesi kwa muda aliopangiwa," alisema Kamwe.

Aucho alicheza mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly nchini Misri na baada ya hapo hakuwapo kwenye kikosi cha Yanga katika michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC na Ihefu FC uliochezwa jana katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

VIPAJI...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gerezani, wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. PICHA: JUMANNE JUMA

# Yanga yalipa kisasi

INATOKA UKURASA 24

lililojaa wavuni.

Winga raia wa Ghana, Okrah aliyeingia kipindi cha pili, aliipatia Yanga bao la nne dakika saba kabla ya mechi kumalizika, alipotanguliziwa mpira mrefu na Aziz Ki, akawatoka na kuwazidi mbio mabeki wa Ihefu kabla ya kuuweka wavuni.

Dakika mbili baadaye, Nzengeli ambaye naye aliyeingia kipindi cha pili, alifunga kitabu cha mabao kwa Yanga, alipoachia shuti kali lililogonga mwamba wa juu na kudunda chini, waamuzi wa mchezo wakaamuru ni bao, ingawa picha za marejeo zilizonyesha mpira ulidunda nje ya mstari wa lango.

Kipindi hicho cha pili kwa nyakati tofauti, Ihefu ilifanya majaribio kadhaa langoni mwa Yanga, lakini wachezaji wao walionekana kutetemeka linapokuja suala la kuuweka mpira ndani ya wavu.

Elivis Rupia ndiye aliyekosa mabao mengi ya wazi, akifuatiwa na Rafael Daudi ambao kama wangetulia wangeweza kufunga mabao katika mchezo huo.

Kipigo hicho kinaifanya Ihefu kushuka kutoka nafasi ya nane hadi ya 10 ya msimamo ikibakia na pointi 23, mabao 18, ikiwa imeshacheza mechi 20 mpaka sasa.

# Kakolanya aianika Simba Ligi Kuu

INATOKA UKURASA 24

wale ambao hawakucheza mechi mbili zilizopita watapata nafasi," alisema Matola huku akiwaita mashabiki kujitokeza uwanjani na kuahidi kuwafurahisha.

Kaimu Kocha wa Ihefu FC, Ngawina, alisema wamefanya maandalizi ya mwisho na wanaifahamu Simba hivyo wamejipanga kulingana na ubora wa wapinzani wao kuhakikisha wanaonyesha mchezo mzuri.

Ngawina alikiri katika michezo minne hawajapata matokeo mazuri, lakini wanaendelea walipoishia wenzake waliopita kuhakikisha wanamaliza dakika 90 kwa kutafuta alama muhimu.

"Tutacheza kwa tahadhari kubwa sana kwa sababu tunafahamu ubora wa Simba ikiwamo safu yake ya ushambuliaji, lakini pia kuna madhaifu yao katika ulinzi tukiwa makini tutawafurahisha mashabiki wetu," alisema Ngawina.

Nahodha wa Singida Fountain Gate FC, Beno Kakolanya, alisema wanaifahamu Simba na wataenda kucheza mechi hiyo kwa tahadhari kubwa kwa kutafuta pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri.

"Niliwahi kucheza Simba, hicho si kigezo kwetu kikubwa, ila nawafahamu wapinzani wetu na tutaingia kwa tahadhari kubwa ili kuweza kuvuna pointi, tukikosa tatu basi tupate moja," alisema Kakolanya.

Michezo

Jumanne Machi 12, 2024

Nipashe



Klopp alia refa kuinyima Liver penalti UKURASA 21

# Yanga yalipa kisasi Ihefu na nyongeza

## ●●● Aucho naye aipa pigo robo fainali CAF huku Gamondi akimbwaga Benchikha kwa...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania, Yanga, wamelipa kisasi kwa Ihefu FC, baada ya kutoa kichapo cha '5G' (mabao 5-0) kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana, huku kiungo mshambuliaji Stephane Aziz Ki, akifunga bao lake la 12 na kumfikia Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC, wote wakiwa kileleni katika mbio za kiatu cha ufungaji bora.

**Yanga ni kama imelipa kisasi na nyongeza juu kwani katika mechi ya mzunguko wa kwanza Oktoba 4, mwaka jana, ilikubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Highland Estates, Mbrali mkoani Mbeya.**

Kiungo huyo raia wa Burkina Faso alitoa pasi tatu za mabao jana, hivyo kufikisha 'assist' tano mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

Aidha, Kiungo mshambuliaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Maxi Mpia Nzengeli, naye alifunga bao moja akifikisha mabao tisa huku Mudathir Yahaya akiendeleza moto wake wa kufunga mfululizo, akipachika bao tena katika mechi ya jana na kufikisha mabao manane.

Pacome Zouzoua naye alifikisha mabao saba akifunga moja, huku Augustine Okrah akifunga bao la kwanza akiwa na timu hiyo msimu huu, baada ya kusajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo.

Ushindi huo unaifanya Yanga kufikisha pointi 49, ikiwa imepachika mabao 47 katika michezo 18 iliyocheza, ikiendelea kuyoyoma na kuziacha timu zingine, na kuonekana kusogelea ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya tatu msimu huu.

Ihefu ndiyo waliouanza mchezo kwa kasi, na sekunde ya 40 tu walikuwa wameshapiga hodi kwenye lango la Yanga, kwa Joseph Mahundi kuambaa na mpira wingi ya kushoto, akapiga krosi ambayo ilikosa muunganishaji, ikaokolewa na mabeki wa Yanga.

Mpira uliookolewa ulimkuta Duke Abuya ambaye shuti lake liliwababatiza walinzi wa Yanga na kumrudia mkononi ikawa faulo. Hilo ndilo shambulizi pekee la hatari kufanywa na Ihefu dakika zote za kipindi cha kwanza.

Yanga ilijibu dakika ya tatu wakati Yao Kouassi alipokimbia na mpira wingi ya kulia na kumimina krosi ambayo ilishindwa kutendewa haki na Pacome Zouzoua ambaye alipiga hewa.

Dakika sita baadaye, Pacome alirekebisha makosa yake alipoukwamisha mpira ndani ya wavu, akimalizia pasi ya juu kutoka kwa Aziz Ki, likiwa ni bao lake saba kwa kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kipa wa Ihefu, Khomein Aboukakar, alifanya kazi ya ziada ya kuruka juu na kuuwahi mpira wa krosi ya Nicson Kibabage, kabla mpira haujamfikia Mudathir dakika 18 ya mchezo, huku mchezaji huyo akikosa bao la wazi dakika ya 25, alipopaisha mpira akiwa ndani ya eneo la hatari, akiunganisha krosi ya Yao.

Mudathir alirekebisha makosa yake dakika ya 29, alipofunga bao la pili, akimalizia pasi mpenyezo ya Aziz Ki.

Kipindi cha pili, Ihefu ilionekana kupoteana hasa kwenye safu ya ulinzi, jambo iliwapa nafasi Yanga kutawala na kuweza kupachika mabao matatu mengine.

Aziz Ki alifunga bao la tatu dakika ya 67 akiwa amezungukwa na mabeki wa Ihefu, ambapo baada ya kupata pasi kutoka kwa Pacome, alizunguka na kuachia shuti dhaifu,

INAENDELEA UKURASA 23



Winga wa Yanga, Maxi Mpia Nzengeli, akimpongeza Stephane Aziz Ki, baada ya kuifungia timu yao bao la tatu wakati wakishinda 5-0 dhidi ya Ihefu FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Kakolanya aianika Simba Ligi Kuu leo

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajia kuendeleza kasi yao ya ushindi kwenye Ligi Kuu Bara baada ya kutoka kuichapa Coastal Union ya Tanga mabao 2-1 ugenini, wapinzani wao katika mchezo wa leo, Singida Fountain Gate FC, wamesema utakuwa mchezo mgumu lakini "tunawafahamu ubora na udhaifu wao ulipo".

Simba itaikaribisha Singida Fountain Gate FC katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, saa 1:00 usiku, ambayo katika michezo sita iliyopita imeambulia sare moja mingine mitano ikichezea kichapo.

Katika mchezo huo, Simba watakuwa nyumbani Azam Complex baada ya Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro kufungiwa kutokana na kutokidhi vigezo vya Bodi ya Ligi nchini.

Timu hizo zote zinakutana kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara bila kuwa na makocha wake wakuu benchini, Abdelhak Benchikha wa Simba akienda kuongeza ujuzi kwa kufanya kozi fupi na kuwaachia wasaidizi wake, Farid Zemiti na Selemani Matola, huku Singida Fountain Gate FC ikiwa imetimua benchi lote la ufundi na Ngawina Ngawina kupewa ukaimu wa kukiongoza kikosi cha timu hiyo.

Kuelekea mchezo huo Kocha Msaidizi wa Simba, Matola amesema maandalizi ya mechi ya leo dhidi Singida Fountain Gate FC yamekamilika na kwamba wanatambua siku zote hakuna mechi rahisi, lakini wamejipanga kulingana na ubora na madhaifu ya wapinzani wao.

Alisema itakuwa mechi ya ushindani kwani Singida Fountain Gate FC siku zote inawapaga wakati mgumu, lakini wamejipanga kuhakikisha wanafanikiwa kuvuna pointi tatu katika mchezo huo wa leo.

"Tumechukuwa tahadhari kubwa katika safu yetu ya ulinzi kwa sababu tukifanya makosa katika nafasi hiyo kwa timu ya Singida Fountain Gate FC basi tunaweza kupoteza.

"Kulingana na ratiba tuliyokuwa nayo, tutakuwa na mabadiliko ya kikosi kwa kuwapa nafasi ya wachezaji wengine kupumzika na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >